# MAFUNDISHO YA BIBLIA KUHUSU UBATIZO

Bobby Jamieson

*Mafundisho Ya Biblia Kuhusu Ubatizo*
Hakimiliki © 2018 Ekklesia Afrika

Haki zote zimehifadhiwa

Kilichapishwa mara ya kwanza kwa lugha ya Kiingereza mwaka wa 2016 na B&H Publishing Group Nashville, Tennessee.

Kuchapishwa mara ya kwanza kwa lugha ya Kiswahili mwaka wa 2018 na Ekklesia Afrika, Nairobi Kenya.

Kutafsiriwa na: Ronald Kogo

Kuhakikishwa na: Milton Isiye na Abel Lugaila

Nukuu za Biblia zimetolewa katika Biblia Habari Njema kwa watu wote, ambayo imechapishwa na Bible Society of Tanzania na Kenya mwaka wa 2001

## Yaliyomo

Maelekezo ya msululu wa vitabu hivi

Utangulizi

**Sura ya Kwanza:** Ubatizo ni nini?

**Sura ya Pili:** Je, ni nani anapaswa kubatizwa?

**Sura ya Tatu:** Je, watoto wanapaswa kubatizwa?

**Sura ya Nne:** Kwa nini ubatizo unahitajika ndipo mtu awe mshirika wa kanisa?

**Sura ya Tano:** Je, ni wakati gani mtu anaweza kubatizwa, lakini awe kweli hajabatizwa

**Sura ya Sita:** Je, ubatizo unapaswa kufanywa kwa njia gani na makanisa?

## Maelekezo ya msululu wa vitabu hivi

Maisha ya mkristo ni maisha anayoishi kwa ufahamu kwamba yeye ni mshirika wa kanisa. Ufahamu huu, ndiyo mwongozo wa msululu wa vitabu tunavyovichapisha. Kwa mfano, kulingana na Biblia, Meza ya Bwana huadhimishwa katika jamii ya kanisa na wala si jukumu la mtu binafsi. Wito wa kusambaza habari njema si jukumu la mtu binafsi, bali ni jukumu lililopewa kanisa kwa jumla. Mamlaka ya kanisa hawajapewa tu viongozi, bali pia washirika wanaitwa kutekeleza mamlaka katika kanisa. Pia, kulingana na Biblia, kila mshirika ana kazi ya kufanya.

Kila kitabu katika msululu wa vitabu vyetu, kimeandikwa kikilenga mshirika wa kawaida. Ikiwa maisha ya mkristo, ni maisha ambayo anaishi akifahamu kwamba yeye ni mshirika wa kanisa, yeye lazima awe amebatizwa na kuletwa katika ushirika wa kanisa. Kwa sababu hii, mshirika ana jukumu la kufahamu mafundisho ya vitabu hivi ambavyo tunavichapa.

Kama tu vile Yesu anaamuru kanisa kueneza na kulinda ujumbe wa injili, vivyo hivyo, anakuamuru ueneze na ulinde watu wake ambao wamezaliwa kwa nguvu za

ujumbe wa injili, yaani kanisa. Msululu wa vitabu hivi vitakueleza wazi jinsi ya kufanya kazi hii.
Wewe unafananishwa na mwekezaji katika huduma ya injili ya Yesu Kristo. Je, mwekezaji hufanya nini? Yeye au wao hujifunza kuhusu biashara, soko na wapinzani wao katika kazi ambayo wanaekeza ndani. Wao hufanya hivi kwa sababu wanataka kupata faida kubwa katika biashara. Mkristo amewekeza maisha yake katika ujumbe wa Injili. Kwa hivyo sababu ya msululu wa vitabu hivi ni kwamba, uweze kuleta mazao mengi katika ufalme wa Mungu kupitia kwa kanisa lako.

Je, uko tayari kuanza kazi yako?

Jonathan Leeman,
Mhariri wa msululu wa vitabu hivi

## Utangulizi

Msomaji wangu, tujifunze kuhusu ubatizo. Kitabu hiki ambacho ni kidogo, kina mambo mengi ambayo ni ya muhimu sana kwako haswa ikiwa wewe ni Mkristo.

Ikiwa wewe umeokoka, ni furaha yangu kwamba unasoma kitabu hiki. Pia kuna vitabu vingi vingine ambavyo ningekuhimiza usome vitabu vinne vya injili na kitabu cha Greg Gilbert ambacho kinaitwa, "Yesu ni nani?" Pia ninakuhimiza kwamba wewe na rafiki wako mchukue muda msome Biblia kwa pamoja, na mjadili kuhusu inamaanisha nini kumfuata Yesu.

Ningependa kuzungmza na mtu ambaye ameokoka lakini hajabatizwa. Huenda hujui ubatizo inamaanisha nini. Pia huenda unajua maana ya ubatizo, lakini unajiuliza kwa nini unapaswa kubatizwa. Labda unajiuliza kama kweli ubatizo ambao ulibatizwa nao, ulikuwa wa kweli! Labda ulibatizwa ukiwa mdogo, na hukumbuki kama kweli ulikuwa umeokoka au la. Kitabu hiki kinashughulikia mambo haya yote.

Kusudi langu ni kwamba, ikiwa wewe ni mkristo lakini hujabatizwa, ninaomba kwamba mafundisho ya kitabu hiki yatakushawishi ubatizwe.

Kikundi cha pili ambacho ninalenga, ni wale wakristo ambao wanataka kujifunza zaidi kuhusu ubatizo. Huenda umebatizwa, lakini unataka kufahamu zaid kuhusu amri hii ya Yesu Kristo kwa kanisa lake. Huenda unataka kuelewa ili uweze kumweleza mwenzako kuhusu jambo hili la ubatizo. Ni ombi langu kwamba kitabu hiki kitaweza kuyajibu maswali yako yote.

Ningependa kikundi kingine kisome kitabu hiki ni wachungaji. Mara kwa mara wachungaji ndiyo huwa wanafanya kazi hii ya kuwabatiza washirika wao. Wachungaji huwa wanawasaidia sana washirika wao kufahamu ubatizo ni nini na unapaswa kufanywa kwa njia gani. Pia wachungaji huwa wanadhihirisha kama kweli mtu kuwa mshirika wa kanisa anahitaji kubatizwa au la.

Ninajua kwamba hatutakubaliana katika mambo yote ya kitabu hiki. Kuhusu ubatizo kuna mambo kadhaa ambayo wakristo huwa hawakubaliani nayo. Lakini ninaomba kwamba kitabu hiki kitakufaidi sana, hata katika yale ambayo hukubaliani nayo.

Katika kitabu hiki, tunauliza maswali, je, ubatizo ni nini? ni nani ambaye anapaswa kubatizwa?, Tutazingatia swali hili, je, watoto wachanga wanahitaji kubatizwa? Pia tunaona ubatizo ambao si wa kweli. Halafu tutatazama jinsi makanisa yanapaswa kuendesha mambo ya ubatizo.

Asante sana kwa kuchukua muda wako na kusoma kitabu hiki. Ninaomba kwamba kitakusaidia katika mwenendo wako na Yesu, na katika kuwasaidia wengine.

Sura ya Kwanza

## Ubatizo ni nini?

Je, utafanya nini ikiwa ulikuwa kando ya bwawa la kuongelea, kisha rafiki yako akuingize katika bwawa hilo? Je, utafanya nini? Utapuuza kitendo chake?

Mfano wa pili, utafanya nini ikiwa rafiki yako atakuja na akuingize ndani ya maji, halafu aseme, "sasa umebatizwa!" Hata kama haujui mengi kuhusu ubatizo, nadhani utakuwa na shauku ya kwamba, ijapokuwa kitendo hicho ni cha nadra sana, rafiki yako atakuwa amekosea. Haujabatizwa; kile ambacho kimefanyika ni kuwa umeingizwa ndani ya maji.

Je, nini kinapaswa kufanyika ndipo ubatizo uwe wa kweli? Ukweli ni kwamba, ubatizo wa kweli si jambo la kushangaza, bali ni jambo ambalo litafanyika ukiwa unajua na ukiwa umejitolea mwenyewe. Je, kuna makanisa ambayo yanawabatiza watoto wachanga? Ukweli ni kwamba watoto huwa hawajitoi kubatizwa, wao hubatizwa bila idhini yao. Je, yule ambaye anabatiza, anapaswa kuwa mchungaji au mtu yeyote? Je, mahali pa

kufanyia ubatizo, panapaswa kuwa wapi, kanisani au mahali pa popote?

**Ubatizo ni……**

Sura hii itajibu swali hili, "Ubatizo ni nini?" Nitaanza kwa kueleza ni nini Biblia inafundisha kuhusu ubatizo, halafu pia nitaeleza mambo machache kuhusu kile ambacho si ubatizo. Kama hajabatizwa kwa sababu haukuwa na uhakika ya ubatizo ni nini, ni tumaini langu kwamba hii sura itakusaidia kufahamu ubatizo na kuweza kutii amri ya Yesu kuhusu ubatizo.

*Ubatizo ni kitendo cha kanisa kuthibithisha na kuonyesha ushirika wa mkristo na Krsito kwa kumzamisha kwenye maji, na pia ni kitendo cha mkristo kudhihirisha hadharani kujitolea kwake kwa Kristo na watu wake, na kwa hivyo kuunganisha mkristo na kanisa na kumtofautisha na dunia.*

Kutokana na maneo haya, tutazame kila mstari jinsi unaambatana na maandiko.

**Kanisa ndilo linabatiza**

Ubatizo ni kitendo cha kanisa. Ubatizo ni jambo ambalo mtu humfanyia mwingine. Mtu awezi kujibatiza mwenyewe, lazima kuwe na vikundi viwili ambavyo vinahusika. Na kila kikundi husema kitu kwa mwingine na kwa dunia.

Watu siku hizi hufikiria ya kwamba ubatizo ni jambo ambalo wanaweza amua kujifanyia, kama kuamua kununua shati kwa dukani. Unaponunua shati dukani, haijalishi nanai anayekuuzia au duka analo nunua shati hiyo. Katika ubatizo, anayebatizwa ndiye huwa tunatilii mkazo sana. Yule anayebatizwa, anapaswa kufanya mwenyewe uamuzi wa kubatizwa, kwa sababu ni yeye ambaye anataka kufanya tangazo kwamba wako pamoja na Yesu. Mfano wa Filipo na Towashi wa Kushi katika Matendo ya Mitume 8, kwa wengi wanaweza kuwaza kwamba ubatizo ni jambo dogo.

Agano Jipya linapeana picha kamili ya ubatizo. Kile ambacho tunakipata katika Matendo ya Mitume 8, siyo jambo ambalo limezingatia sana katika maandiko ya Biblia yote. Haufai kuanza katika Matendo ya mitume kuhusu jambo la ubatizo, bali katika injili ya Matayo 16

na 18. Katika vifungu hivi, Yesu amekabidhi funguo vya ufalme kwanza kwa mitume halafu kwa kanisa. Funguo vya Ufalme ni vya kufungu duniani kilicho fungwa mbinguni, na kufungua dunia kile kilicho funguliwa mbiguni.  Hii inamanisha ya kwamba, mitume walikuwa na mamlaka kutoka kwa Yesu kuamua kwa niaba ya Yesu. Leo mamlaka hayo yamekabidhiwa kanisa. Waza ya hakimu anapokuwa anatoa uamuzi wake. Yeye huwa anatoa uamuzi huu kulingana na sheria ya nchi. Yeye ni mwakilisha wa nchi kutekeleza sheria ya nchi.

Mamlaka ya kufanya tangazo maalumu kwa niaba ya mbinguni, ni jambo ambalo Yesu amelikabidhi kanisa, siyo mtu binafsi. Matayo 18:20: “Kwa maana wanapokutana watu wawili au watatu katika jina langu, hapo mimi nipo pamoja nao.” Hapa, Yesu haongelei kikundi cha watu wachache, ambao kuwepo kwake Yesu miongoni mwao ni jambo ambalo halieleweki. Kanisa ni mukutano wa mara kwa mara wa watu wawili au watatu wanaokiri jina la Kristo. Kristo yuko pamoja na kusanyiko hilo na amewapea mamlaka ya kuzungumza kwa jina lake.

Tunahitaji kuelewa haya yote, ndipo tuelewe kazi yetu ya kuyafanya mataifa kuwa wanafunzi wa Yesu katika

Matayo 28. Kwanza Kristo anatukumbusha kuwa Yeye ndiye aliye na mamlaka mbiguni na duniani (mstari wa 18). Baadaye ya hayo maneno, anawamuru wanafunzi wake kufanya watu wengine kuwa wanafunzi wake na kuwabatiza kwa Jina la baba, Mwana na Roho Mtakatifu. Halafu anawaambia wafundishe kila kitu ambacho amewamuru, kazi hii hii inaendeleshwa na kukamilishwa katika kanisa. Mwisho anawahakikishia kwamba atakuwa pamoja nao wakati wanapokuwa wanafanya kazi hii: “ Nami nipo pamoja nanyi siku zote; naam, mpaka mwisho wa nyakati. Mafundisho ya Mathayo 16, 18 msingi wake uko katika mafundisho ya Mathayo 28.

Ni nani anayo mamlaka ya kubatiza? Je, mkristo yeyote? Ikiwa uko kwa kazi ya kuhubiri injili mahali ambapo hakuna wakristo wengine, itabidi ufanye kazi hiyo ya ubatizo kwa wale ambao wanaokoka. Utafanya hivyo kwa sababu mahali hapo hakuna kanisa. Matendo ya Mitume 8 inatoa mfano kwako kama utawahi kuwa katika hali hiyo. Wakati huo huo, kumbuka kwamba Yesu amehusisha wazi wazi uwepo wa mamlaka kwa makanisa na watu wawili au watatu wanaokusanyika kwa jina lake. Kwa kawaida ni kanisa ambalo lina mamlaka ya kubatiza. Ubatizo hufanywa na mtu mmoja, kwa niaba ya kanisa. Kanisa hubatiaza kupitia kwa mwakilisha wake ambaye

anaeze kuwa mchungaji au mtu ambaye kanisa litamchangua.

Kanisa halina mamlaka ya kukataa kumbatiza mtu ambaye anakiri kuokoka na anaonekana kuishi kulingana na kukiri kwake (Matendo Ya mitume 11:17-18). Lakini pia ni vyema kufahamu kwamba, kanisa linahusika kwa sababu tangaza la ubatizo wa mtu, pia ni ushuhuda mkubwa wa kanisa kwa wale ambao hawajaokoka. Kanisa linaakilisha mbingu hapa duniani.

**Ubatizo huthibitisha na kuonyesha kwamba mwenye kubatizwa, ameungana na Kristo**

Je, ushuhuda wa kanisa katika kubatiza ni wa aina gani? Kwa kuwa ubatizo wa kanisa huthibitisha imani ya ya Yule ambaye anabatizwa, kwamba yeye yuko ndani ya Kristo. Huthibitisha ya kuwa yule ambaye anasema ya kwamba umeunganika na Kristo katika ufufuo wake, ni mkristo. Kanisa huweka muhuri unaoonekana kwa wote.

Imani hutuunganisha kwa Kristo ndipo tuweze kuona manufaa ya kifo na ufufuo wake. Ubatizo ni ishara ya muungano huo.

“Maana , mnajua kwamba sisi tuliobatizwa tukaungana na Kristo Yesu, Tulibatizwa na kuungana na kifo chake. Tulipobatizwa tuliungana na kifo chake, tukazikwa pamoja naye, ili kama vile Kristo alivyofufuliwa kutoka wafu kwa kitendo kitukufu cha baba, sisi pia tuweze kuishi maisha mapya.” (Warumi 6:3-4)

“Tangu kufika kwa hiyo imani, sheria si mlezi wetu tena. Kwa njia ya imani, ninyi nyote mmekuwa watoto wa mungu katika kuungana na Kristo. Ninyi nyote mliobatizwa mkaungana na Kristo ni kama vile mmemvaa Kristo.” (Wagalatia 3:25-27)

Ubatizo ni ishara ya kazi ya injili katika maisha ya mtu. Ni ishara ya kwamba umeacha dhambi na akaunganika kwa Kristo kwa imani. Ubatizo haudhihirishi kukiri tu, bali pia kazi ya Mungu katika maisha ya mtu. Waza juu ya kifo, kuzikwa na kufufuka kwa Yesu. Ubatizo hudhibitishia wale ambao wanashuhudia muangano wa mtu na kifo, kuzikwa, na ufufuo Yesu Kristo. Mtu huingizwa kimwili kwa maji na kuinuliwa kutoka kwa maji. Ishara ya kufa kwa dhambi na kufufuka kwa maisha mapya ndani ya Yesu Kristo.

Ubatizo huonyesha kuungana kwetu na Kristo, na manufaa ya hiyo muungano. Kupitia kwa Kristo dhambi zetu zinasamehewa na Kuoshwa. Ubatizo unaonyesha mambo haya yote. Petero aliuambia umati siku ya pentecoste, “Tubuni na kila mmoja wenu abatizwe kwa jina la Yesu Kristo ili mpate kuondolewa dhambi zenu na kupokea ile zawadi ya Roho Mtakatifu (Matendo ya Mitume 2:38). Anania alimwambia Paulo, “Sasa basi, ya nini kukawia zaidi? Simama ubatizwe na uondolewe dhambi zako kwa kuliungama jina lake” (Matendo ya Mitume 22:16). Katika Kristo tunapata maisha mapya ambayo yamejazwa na nguvu za Roho Mtakatifu. Mfano wa kutolewa ndani ya maji wakati wa ubatizo, inaashiria haya maisha. (Warumi 6:4; Wakolosai 2:11-12). Katika ubatizo kanisa linathibitisha ya kwamba yule mtu ambaye anakiri imani katika Kristo ameunganika na Kristo, na inaonyesha huo muungano na manufaa yake.

**Wakati wa ubatizo, mtu huzamishwa ndani ya maji**

Je, kanisa hudhihirishiaje mtu kwamba amefufuka kutoka kwa dhambi na yuko hai katika Kristo? Jibu ni kwamba, kwa kumuzamisha kwa maji. Neno la kigiriki “baptize”, ambalo neno letu “ubatizo” hutoka, linamanisha kuingiza au kurusha kitu ndani ya maji, kwa kawaida kusababisha

kuzama kabisa. Biblia katika Agano Jipya inafundisha na kuonyesha kwamba ubatizo ni kuzamishwa. Yohana mbatizaji alibatiza “huko Ainoni karibu na Salimu kwa sababu huko kulikuwa na maji mengi” (Yohana 3:23), na hakuna ishara ya kwamba ubatizo uliyofanywa na wanafunzi wa Yesu ulihataji maji kidogo.

Zaidi, wakati Towashi wa Kushi aliweka imani yake katika Kristo, alimwabia Filipo, “Tazama, hapa kuna maji! Kuna kitu gani cha kunizuia mimi nisibatizwe?” (Matendo ya Mitume 8:36). Na tunasoma, “Akaamuru gari lisimamishwe. Wakateremka, yule Towashi na Filipo, wakaenda pale kwenye maji. Filipo akambatiza. Walipotoka katika yale maji, Roho wa Bwana akamchukua Filipo na yule Towashi hakumwona tena. Kwa hiyo akaendelea na safari yake akiwa amejawa na furaha” (Matendo ya Mitume 8:38-39). Inaonekana ya kwamba ubatizo ulihitaji maji mengi kushida yale walikuwa nayo kwenye gari, kwa hivyo iliwabidi washuke ndipo wafanye ubatizo.

Hatimaye, maelezo ya Paulo ya kwamba ubatizo huashiria kifo, kuzikwa na kufufuliwa na Kristo, kwa yule anaye batizwa. Katika Warumi 6:1-4, ni wazi kwamba kubatizwa ni kuzamisha. Kuzamishwa kimwili huonyesha

kuzikwa, kutolewa huonyesha kufufuliwa na kuunganishwa na Yesu Kristo. Kwa hivyo kanisa linathibitisha na kuonyesha kuungana kwa aliyeamini pamoja na Kristo.

**Ni tendo la mkristo**

Lakini ubatizo siyo tendo la kanisa pekee, pia ni tendo la mkristo. Kanisa hubatiza, Mkristo anabatizwa. Fikiria jinsi wale waliomsikiliza Petero wakati wa pentencoste walifanya.

Watu waliposikia maneno haya yaliwachoma moyoni, wakawauliza Petro na wale mitume wengine, “Tufanye nini ndugu zetu?” Petro aliwajibu, “Tubuni, muache dhambi na kila mmoja wenu abatizwe katika jina la Yesu Kristo, ili msamehewe dhambi zenu; nanyi mtapokea zawadi ya Roho Mtakatifu. Kwa maana ahadi hii ilitolewa na Mungu kwa ajili yenu na watoto wenu, na wale wote walio nchi za mbali, na kila mtu ambaye Bwana Mungu wetu anamwita kwake.”...Wote waliopokea ujumbe wa Petro walibatizwa na zaidi ya watu elfu tatu wakaongezeka katika kundi la waamini siku hiyo.

Wale waliotubu dhambi zao na kumuamini Yesu Kristo walibatizwa.Ubatizo ndiyo tendo la kwanza la hadharani linalodhihirisha imani ya kumpokea Yesu kama Bwana na mwokozi wa maisha yetu. Kama wewe ni Mkristo, Yesu anakuamru ubatizwe. Ni kitu ambacho ni lazima ufanye; hakuna mtu yeyote anaweza kukufanyia.

Wale ambao hawajaokoka, hawafai kubatizwa. Ubatizo unathibitisha na kuonyesha muungano wa mkristo na Krsito, kwa hivyo ni wale tu ambao wameunganika na Kristo kwa imani wanastahili kubatizwa.

**Ubatizo ni kitendo ya Yule aliyeokoka kujitolea hadharani kwa Kristo**

Mkristo hufanya nini katika suala la ubatizo? Huwa anajitolea hadharani kwa Kristo. Ubatizo ni njia ya kuonyesha hadharani kuwa umekuwa Mkristo. Ni jinsi unavyokiri imani yako, kwa kunyenyekea kwa Bwana Yesu Kristo.

Kwa ajili ya kuitikia wito wa injili, tumeamuriwa kumfuata Yesu kwa matendo ya nje na ndani. Matendo ya nje hutangaza kile tulichonacho ndani yetu. Ubatizo hufanywa wazi, mbele ya mashhaidi. Waza juu ya wale

waliotubu na wakabatizwa wakati wa pentecoste. Wale wote walijitokeza  kutoka kwa umati wa watu wabatizwe walikuwa wanaashiria kuwa wamekuwa wafuasi wa Yesu.

Wafuasi wa Kristo wanapaswa kuwa watu ambao wanaonekana na kila mtu. “Kila mtu atakayenikiri mbele ya watu, mimi pia nitamkiri mbele ya Baba yangu aliye mbinguni. Lakini yeyote atakayenikana mbele ya watu, mimi pia nitamkana mbele ya Baba yangu aliye mbinguni” (Mathayo 10:32-33). Hakuna wanafunzi wa Yesu wa kisiri. Njia ya pekee ya kumfuata Yesu ni kufanya hivyo hadharani, mahali ambapo kila mtu anaweza kukuona.  Na ubatizo ndiyo njia ambayo tunatangaza mbele ya kanisa na dunia yote kuwa sisi ni watu wa Kristo. Yesu anataka wanafunzi wake waangaze ndipo ulimwengu umwone kupitia kwao. Ubatizo ndiyo njia ya kuingia katika hiyo mwanga.

Kama uko na wasiwasi juu ya kutangaza imani yako hadharani, angalia ubatizo kama usaidizi na siyo kiziizi. Yesu ajaacha utegemee ujasiri wako ama ubunifu wako kujua jinsi utakavyojitangaza umekuwa mkristo; amekuonyesha njinsi ya kufanya hivyo. Ameifanya iwe

rahisi! Kile unafaa kufanya ni kukiri tu imani yako kwa Kristo.

Ubatizo siyo tu kukiri kwamba umeokoka, ubatizo ni kufanya uamuzi wa kujitolea kwa Yesu Kristo. Petro anaandika jinsi ambavyo Noa na familia yake walivyookolewa kutoka kwa ghadhabu ya Mungu katika gharika. Petero anafananisha hili na  “Maji hayo ni kielelezo cha ubatizo ambao sasa unawaokoa ninyi, si kwa kuondoa uchafu kwenye miili yenu, bali kama dhamana ya kuwa na dhamiri njema kwa Mungu kwa ajili ya kufufuka kwa Yesu Kristo” (1 Petro 3:21). Wakati ambapo Petro anasema kuwa ubatizo “huokoa,” anafafanua kuwa kile inaokoa siyo kuoshwa mwili na maji, bali ni imani ambayo ubatizo inadhihirisha. Kwa imani tunampokea Kristo aliye fufuliwa, halafu tunabatizwa.

Maneno haya, “ahadi ya dhana mzuri” inaweza chukuliwa kama maombi ama ahadi, ama zote. Nafikiri mambo haya yote yanapatikana katika ubatizo, hata kama mstari huu unasisitiza moja ama nyigine. Ubatizo ni maombi ambayo hutoa sauti kwa ombi la imani “niokoe, Bwana Yesu!” Kwa kujitabulisha na kifo na ufufuo wa Yesu Kristo katika ubatizo, mkristo husema kwamba Kristo ni

mwokozi wake. Yeye huwa anamlilia Mungu, kwamba awe mkristofu kwa ahadi zake.

Kubatizwa ni kujitoa kabisa, na kunyenyekea kwa Kristo kama Bwana. Kubatizwa kwa jina la Kristo (Mathayo 28:19) ni kunyenyekea kwa uongozi wake. Ubatizo ni kiapo ya kutii mfalme Yesu. Ni kuhapa kwamba tutakuwa waaaminifu kwake. Ubatizo ni ahadi ya kutii amri zote za Kristo. Kubatizwa ni alama ya kuti amri "Yashikeni mambo yote niliyowaamuru ninyi" (Mathayo 28:20). Hauwezi kumpokea Yesu kama mwokozi na ukose kumheshimu kama Bwana. Katika ubatizo tunauchukuwa msalaba wa Yesu na kutembea katika njia zake.

Ubatizo ni dhihirisho la hadharani la imani. Ni mahali ambapo tunavaa mavazi ambayo yanatutambulisha pamoja na Yesu. Ubatizo kwa mkristo ni kusema kwamba Yesu Kristo ni mwokozi wake na anajitoa kunyenyekea kwake kama Bwana.

**Ni tendo la kanisa**

Katika ubatizo mkristo hujitolea siyo tu kwa Kristo pekee, bali pia kwa watu wa Kristo. Kumbuka tena kilichofanyika wakati wa pentecoste: "Wale wote

waliopokea ujumbe wa Petro kwa furaha wakabatizwa na siku ile waliongezeka watu wapatao 3,000” (Matendo ye Mitume 2:41). Hawa wapatao 3000 waliogezewa kwa nani? Kwa kanisa la Yerusalemu, ambapo hapo awali walikuwa watu 120 (Matendo ya Mitume 1:15). Wale waliobatizwa wakati wa pentecoste walijitoa kutoka kwa ulimwengu wakaingia ndani ya kanisa. Na hivyo ndivyo ilivyo, au inafaa kukuwa kwa kila mtu anaye batizwa leo.

Kumkristo Yesu ni kujiunga na kikundi cha wale ambao wanamkristo. Kumpokea Yesu ni kupokea watu wake. Injili haituleti kwa Mungu peke (Waefeso 2:1-10), bali inatuunganisha na kila mmoja ambaye ni wa Mungu (Waefeso 2:11-22). Kumwita Mungu baba ni kukubali wale wote ambao pia wanamwita baba na kuwachukuwa kama ndungu wa jamii moja. Kuunganishwa na Kristo ni kukuwa mmoja wa mwili wake (1 Wakorintho 12:12-26; Waefeso 1:23; Wakolosai 1:18, 1 Petro 2:10).

Kwa hivyo katika ubatizo, mkristo hujitolea kwa Kristo na kanisa lake, kwa kuvaa fulana ya timu fulani, ni kujitolea kuchezea timu hiyo. Katika ubatizo, unatangaza kutoka katika ulimwengu na unaingia na kujiunga na kanisa. Huwezi sema umeokoka, umebatizwa, lakini hutaki kujiunga na watu wa Mungu. Ubatizo basi, ni

kujitolea kumfuata Yesu pamoja na kanisa lake. Katika ubatizo mkristo hujitolea kupenda, kutumikia na kunyenyekea kwa watu wa Kristo.

**Kuunganisha mkristo na kanisa, na kumtoa katika ulimwengu**

Katika ubatizo, kanisa huwa linatangaza hali yake kwa ulimwengu. Tendo la ubatizo linaonyesha kujitolea kwa mkristo, “Mimi hapa najitolea kwa Kristo na kwenyu, watu wake” na inaonyesha kujitolea kwa kanisa, “Sisi hapa tunathibitisha imani yako na tunajitolea kwako, mmoja wa mwili wa Krsito.” Katika ubatizo, mkristo anaongea na Mungu na Kanisa, na kanisa huongelesha mkristo kwa niaba ya Mungu.

Kwa hivyo, wakati kanisa linathibitisha na kuonyesha imani ya mkristo katika Kristo, na mkristo anajitolea kwa Kristo na watu wake, mkristo anaungana na kanisa na anaondelewa katika ulimwengu. Mkristo anaogezwa kwa kanisa na anapewa vazi lake la kuwa mmoja na watu wa Mungu. Ubatizo huonyesha hadharani kuwa mtu ni mkristo. Katika ubatizo, kanisa huambia ulimwengu, “Tazama hapa! Huyu ni wa Yesu.” Kwa sababu ubatizo huonyesha kuwa mtu ni mkristo, huwa mtu huyu

anaongezeka kwa kanisa, watu wa Agano Jipya la Kristo hapa duniani.

Kuna mengi kuhusu kazi ya ubatizo ambapo mkristo analetwa kuwa mmoja wa kanisa na kumuondoa kwa ulimwengu katika sura ya 4. Kwa sasa, imetosha kuona ya kwamba katika ubatizo mkristo hujitolea siyo kwa Kristo peke bali pia kwa watu wa Kristo.

**Ubatizo siyo….**

Acha tuangalie kwa ufupi maoni juu ya yale ambayo ubatizo siyo. Kwanza, ubatizo si njia ya kupata wokovu. Kumbuka kwamba katika 1 Petro 3:21, Wakati Petro alisema ya kwamba ubatizo si njia ya kupata wokovu, ubatizo huonyesha imani katika kifo na ufufuo wa Yesu. Tunaokoka kwa kuamini katika kifo na ufufuo wa Yesu, ubatizo ni kielelezo na mahali ambapo hiyo imani inadhihirishwa hadharani.

Maandiko yako wazi, *kupitia kwa imani*, dhambi zetu zinasamehewa, tunahesabiwa watakatifu na Mungu, na tunapatanishwa na Mungu (Warumi 3:21-31;4:1-8;5:1-11). Ubatizo huonyesha alama hizi ambazo ni ukweli wote. Lakini siyo ubatizo ndiyo hufanya ukweli huu, uwe

ukweli. Wakristo wote wameamurishwa wabatizwe. Kutii amri ya Yesu ni ishara kwamba imani yetu ni ya kweli (John 14:21-24; Yakobo 2:14-26; 1 John 2:3-6). Kwa hivyo hakuna mkristo anastahili kukataa kubatizwa kwa msingi ya kuwa "siyo muhimu kwa wokovu." Kama unadai ya kuwa umeokoka, ubatizo ni ushahidi. Kubatizwa hakumfanyi mtu kuwa mfuasi wa Yesu. Mwizi msalabani alienda mbiguni bila kubatizwa (Luka 23:39-43), Na Simoni mchawi alikuwa anaelekea kuzimu ilhali alikuwa amebatizwa (Matendo ya Mitume 8:13-14).

Pili, ni muhimu kutambua ya kwamba ubatizo siyo tu tamaduni ya mwanadamu. Siyo kitu ambacho kanisa lilibuni. Siyo kitu ambacho sisi wakristo tunafanya tu na tunaweza tu kukosa kufanya. Badala yake, ni amri kutoka kwa Kristo ambayo inawatambulisha wakristo wote popote walipo.

**Yanayofuata**

Wacha nirudi kwa yule rafiki yako. Je, ikiwa atafaulu kukuzamisha kwa maji, atakuwa amekubatiza?

Hapana, ni tumaini langu kwamba sasa upate kufahamu vyema kutoka kwa Biblia ubatizo ni nini. Katika ubatizo,

Kristo amewapatia wanafunzi wake njia ya wazi ya kujitambulisha pamoja na Yeye. Pia katika ubatizo, Yesu amepeana kanisa lake njia ya kuthibitishia na kuonyesha kwamba kweli mtu ameokoka. Kwa hili tendo la ubatizo, Mkristo hujitolea kwa kanisa na kanisa hujitolea kwa mkristo. Ubatizo ni ishara ambayo inaonyesha muungano wa Mkristo na Kristo na huleta muungano mpya, ya kuunganisha mkristo na kanisa.

Ubatizo ni nini? Sema pamoja nami: *Ubatizo ni kitendo cha kanisa kuthibithisha na kuonyesha ushirika wa mkristo na Kristo kwa kumzamisha kwenye maji, na pia ni kitendo cha mkristo kudhihirisha hadharani kujitolea kwake kwa Kristo na watu wake, na kwa hivyo kuunganisha mkristo na kanisa na kumtofautisha na dunia.*

## Je, ni nani anapaswa kubatizwa?

Je, wewe ni mkristo? Ikiwa wewe mkristo, ninafuraha kwamba unakisoma kitabu hiki. Unapaswa ujue kwamba, jukumu lako la kwanza si kubatizwa. Kile unahitaji kufanya ni kugeuka kutoka kwa dhambi zako na kumgeukia Kristo kwa imani.

Ni ombi langu kwamba wewe unaposoma kitabu hiki umeokoka. Je, ikiwa umeokoka, umebatizwa? Ikiwa bado, kwa nini? Na ikiwa umebatizwa, kwa nini ulibatizwa?

Je, ni “Nani anapaswa kubatizwa?” Jibu ni, “kila mkristo!” Katika sura hii nitaonyesha mamlaka ya ubatizo kutoka kwa bibilia, nitaangalia manufaa ya ubatizo, na nitajibu pingamizi ambazo huzuia watu kubatizwa. Moja ya hizi pigaminizi ni kuwa mtu “alibatizwa” akiwa mtoto mchanga.

## Mamlaka ya ubatizo

Kama tulivyo angalia katika sura uliyopita, Yesu ameamru wanafunzi wake wafanye wanafunzi wengine. Biblia inasema, “Yesu akawajia na kusema, “Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Kwa sababu hii, enendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa Jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu,nanyi wafundisheni kuyashika mambo yote niliyowaamuru ninyi. Hakika mimi niko pamoja nanyi siku zote, hadi mwisho wa nyakati” (Mathayo 28:18-20). Wanafunzi wa Yesu walifanya aje ndipo wakaweza kuwafanya wengine wanafunzi? Kwanza, kwa kuwahubiria injili ya ufalme, kama vile Yesu alifanya (Mathayo 4:17,23), na kama vile alivyokuwa ametuma wanafunzi wake wafanye (Mathayo 10:5-7). Kwa hivyo ni haki kusema amri “wafanye wanafunzi” inaashiria kuhubiri injili. Unakuwa wanafunzi wa Yesu kwa kutii ujumbe wa Injili.

Lakini Yesu anasema hatua zingine mbili katika utaratibu huo, njia mbili ambazo mamlaka ya kufanya wanafunzi inafaa kufanyika. Wanafunzi wa Yesu wanastahili kubatiza hawa wanafunzi wapya na kuwafundisha kutii yale yote Yesu anaamuru.

Hatua 1: Hubiri injili.

Hatua 2: Watu wanapotii, uwabatize.

Hatua 3:Wafundishe kila kitu ambacho Yesu aliamuru.

Wale wote walikuwa wanafunzi wanabatizwa. Hakuna kikundi cha wanafunzi ambacho hawajabatizwa.

Ubatizo ni kitu ambacho kila mwanafunzi anafaa kufanya, akijitolea kwa hii ishara ya kifo na ufufuo. Kwa hivyo inakaa wazi kutoka na mpangilio ya misemo za yesu ya kwamba ubatizo ni kitu cha kwanza kwa orodha ya "kila kitu nimewaamuru". Baada ya kutubu na kuamini, ubatizo ndiyo amri ya kwanza wafuasi wa yesu wameitwa kutii. Kama mwanafunzi mpya wa yesu, ubatizo ndiyo kitu ambacho kinachostahili kufanyika.

Kwa hivyo, siyo mshangao, kuwa Petro aliwaambia wale walikuwa wakimusikiza wakati wa Pentecoste kutubu na wabatizwe: "Petro akawajibu, "Tubuni, mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina la Yesu Kristo, ili mpate kusamehewa dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu" (Matendo ye Mitume 2:38). Na tumeona ya kuwa wengi wao walifanya hivyo: "Wale wote waliopokea ujumbe wa Petro kwa furaha wakabatizwa na

siku ile waliongezeka watu wapatao 3,000" (Matendo ya Mitume 2:41). Tena, kukubali injili na kubatizwa huambatana pamoja. Ukimwamini Kristo Yesu, kitu ya kwanza unafaa kufanya ni kubatizwa.

Hii pia inaeleza kwa nini waandishi wa barua katika agano jipya walidhani kuwa wasomaji wao ambao ni wakristo walikuwa wamebatizwa. Paulo anasema wale waliokufa kwa dhambi hawawezi tena ishii ndani ya dhambi, halafu anauliza, "Au hamjui ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake?" (Warumi 6:3). Na Paulo anawahakikishia wagalatia ya kuwa hao ni wana wa Mungu kupitia kwa imani kwa Kristo, halafu anawaelezea, "Kwa maana wote mliobatizwa ndani ya Kristo, mmemvaa Kristo" (Wagalatia 3:27;cf. I Wakorintho 1:13; Wakolosai 2:12). Hiyo hoja itafanya tu kama wasomaji wote walikuwa wamebatizwa.

Kama wewe ni Mkristo na haujabatizwa, unahitaji kubatizwa. Siyo kitu cha hiari au ile iliyopedekezwa au jambo la hekima au kitu ya maana ya kufanywa. Inahitajika. Na ilhali kuwa mwanafunzi wa yesu inamaanisha zaidi ya kufuata amri zake, haimanishi kuwa kufuata amri siyo kitu cha maana. Wale wameweka imani

yao kwa Yesu hufanya kile ambacho yeye husema, na amewaamuru wale wanaomuamini wabatizwe.

## Manufaa ya Ubatizo

Kama unadhani ya kwamba umemwamini Yesu, Yesu anakuamuru ubatizwe. Lakini kama bado uko na shauku, nataka kukuhimiza kutii amri ya Yesu ya kubatizwa kwa kukuonyesha manufaa mawili ya ubatizo.

Ya kwanza ni kuwa kukiri imani hufanya imani kuwa na nguvu. Ubatizo ni tangazo la wazi kuwa wewe ni wa Yesu. Na kama bado unasita kutangaza wazi kuwa wewe ni mfuasi wa Yesu, basi ubatizo ndiyo kitu unahitaji kufanya!  Imani katika Yesu inafaa kukufanya uwe kiumbe kipya. Hili tangazo la kweli  kuhusu maisha yako ya zamani, ya sasa, na yajao, familia yako ni nani, na nani anakutii zaidi. Ubatizo unadhihirisha huu ukweli wote.

Kama utajaribu kuficha imani yako, utakufa. Kama miili yetu, imani hutiwa nguvu kwa kufanya mazoezi, na ubatizo ni zoezi ya imani. Ubatizo ni hatua ya imani, na ni hatua ambao huweka muelekeo kwa maisha yetu yote ya imani. Kuwa mkristo ni kuweka wazi maisha yetu ya ukristo. Maisha ya ukristo ni maisha ambayo mtu huishi

kwa uwazi, pamoja na kanisa mbele ya ulimwengu. Na ubatizo ni njia ya kuchukua hatua ndani ya uangalizi.

Manufaa ya pili ni kwamba ubatizo huleta nafasi ya uinjilisti. Familia na marafiki wengi ambao huwa kwa kawaida hawaendi kanisani wanaweza hudhuria ubatizo. Kama wangeni wako hawajui maana ya ubatizo, tumia injili kuwaelezea; Kama hawaelewi injili, tumia ubatizo kuwaonyesha injili. Kama vile unazamishwa kwa maji na kuinuliwa tena, ndiyo yesu alikufa na akashinda kifo. Na wale wote ambao wameunganika na Kristo hushiriki kwa huo ushindi, kwa sababu kupitia kwa njia kifo na ufufuo dhambi zetu zimesamehewa na tunapataniswa na Mungu.

**Pingamizi za Kubatizwa**

Kama unakiri kwamba wewe ni Mkristo lakini haujabatizwa, kwa nini? Wacha tuangalie pingamizi za kubatizwa.

Kwa nini nafaa kufanya ukristo kuwa kitu cha hadharani? Kwani imani siyo kitu cha kibafsi na ya siri? Haitoshi kuwa nimemkristo yesu? Mungu anajua roho yangu. Tumeshaona kuwa yesu hatakuwa na wafuasi wa kibnafsi, hakuna wanafunzi wa siri: “Kila mtu atakayenikiri mbele

ya watu, mimi nami nitamkiri yeye mbele za Baba yangu aliye mbinguni. Lakini yeyote atakayenikana mimi mbele ya watu, mimi nami nitamkana mbele za Baba yangu aliye mbinguni" (Mathayo 10:32-33). Na tena, "Mtu yeyote akinionea aibu mimi na maneno yangu, Mwana wa Adamu naye atamwonea aibu atakapokuja katika utukufu wake na katika utukufu wa Baba, pamoja na malaika watakatifu" (Luka 9:26). Wakristo ni wale ambao wanakiri imani zao kwa Kristo. Ufafanuzi wa kukuri, ni tendo la hadharani, ni kuongea kama mtu anakusikiza, anagalia ubatizo kama kitu cha msaada bali siyo kizuizi. Kubatizwa unakusaidia kufanya kwa imani yako kile unafaa kufanya nayo: Kuitangaza wazi wazi.

Neno kwa viogozi wa kanisa: Nafikiria ni vizuri kufanya mazoea ya kuwauliza wale wanaobatizwa siyo tu kukiri imani yao kwa Kristo na kuahidhi kumtii, lakini pia kueleza njisi wao kibinafsi walimkristo Yesu kama Mwokozi wao. Hii humpatia Mungu utakufu kwa kazi ambayo anafanya katika maisha yao na kufanya ubatizo kuwa na nguvu ya uijilisti. Lakini kama mtu ana hofu ya kushuhudia kwa wote, ninakuhimiza umsihi mtu huyo ashuhudie imani yake na ajitolea kumtii Yesu.

“Unakiri imani yako kwa Kristo Yesu kama Mwokozi wako na kunyenyekea kwake kama?” Bwana.
“Ndiyo”
“Unaahidi, kulingana na neema yake, kumtii Yesu kwa kujumuika na kanisa lake siku zote za maisha yako?”
“Ndiyo”

Nimekuwa mkristo kwa miaka mingi sasa, sikuwa nimebatizwa, kwa nini nibatizwe sasa baada ya hii muda yote? Juu imekuwa muda mrefu tangu nibadilishwe, hata hivyo ubatizo haitakuwa na maana? Ingekuwa vizuri kama ungebatizwa haraka baada ya kukiri imani yako kwa Kristo. Lakini katika kufuata amri za Kristo, afadhali kuchelewa kutii kuliko kutotii kabisa (Mathayo 21:28-32). Na wakati ambayo imepita haifanyi amri kutokuwa ya kufunga. Hakika, kubatizwa saa hii itamaanisha wewe kukubali kuwa ulikuwa umekosea kwa kutobatizwa muda huu wote. Lakini hiyo ndiyo maana ya kumfuata Yesu. Kama tutapata dhambi kwa maisha yetu, tanatubu na kutii. “Sikuja kuwaita wenye haki, bali wenye dhambi wapate kutubu” (Luka 5:32).

*Sijui pa kwenda ili nibatizwe.*

Hiyo inaonyesha kuna shida! Hii ndiyo Mawaidha yangu: tafuta kanisa ambao inahubiri injili na inafundisha biblia. Tafuta kanisa ambao watu wanachukulia maanani kumufuata Yesu na kusaidia wengine kumfuata yesu. Jitabulishe kwa viongozi wa kanisa hilo. Acha wajua kwamba wewe umemkristo Yesu na unataka kubatizwa. Na ujitole kuungana na hilo kanisa, ukitumikia katika kanisa na kuacha kanisa ikusaidie ukue katika mfano wa Kristo. Kama unahitaji msaada ya kutafuta kanisa, unaweza angalia kivutio cha cha kitabu cha Alama 9.

*Nilikuwa nimebatizwa kama mtoto mchanga.*

Ubatizo ni kitu inafanyika mara moja. Kama ulikuwa umebatizwa hauitajiki, na haufai kubatizwa tena. Lakini watoto wachanga wanastahili kubatizwa? Ubatizo wa watoto ni ubatizo kweli? Hili ndilo tutakalojadili katika sura inayofuata.

**Cha Muhimu**

Ikiwa umekuwa ukiharisha ubatizo juu ya wasiwasi ama uoga, usijali. Yesu alifundisha kwamba mtapelekwa na kustakiwa mahakamani kwa ajili yake, na Roho Mtakatifu

atatupatia maneno ya kusema (Mathayo 10:19-20). Je, ni namna gani Roho Mtakatifu atatuwezesha kukiri iamni yetu? (1 Wakorintho 12:3)

Cha maana ni hiki, kila Mkristo ameamurishwa ubatizwe. Wewe unangoja nini?

Sura ya Tatu

## Je, watoto wanapaswa kubatizwa?

Tutasema aje kuhusu kubatiza watoto wachanga? Ni uhakika ya kwamba watu wengine wanaosoma hiki kitabu walibatizwa wakiwa watoto wachanga na kwa sasa wanashauku juu ya hiyo ubatizo. Au unaweza kuwa unajua kanisa ambazo hubatiza watoto wachanga na haujawahi tilia manani au kuchunguza hilo zoezi kulingana na maandiko ya bibilia.

Katika sura hii tutaweka wazi dhana za mafundisho ya theologia ambazo zinaunga ubatizo wa watoto wachanga, halafu tutazikangua kulingana na bibilia, na tutajibu pingamizi kuhusu ubatizo wa wakristo na  wale wanaunga mkono ubatizo za watoto.

### Ubatizo wa watoto wachanga

Katika Historia ya kanisa, kumekuwa makanisa ambayo yamebatiza watoto wachanga. Kuna sababu tofauti ambazo makanisa  hutumia kuunga mkono kubatiza watoto wachanga. Makanisa mengi huamini ya kwamba

ubatizo kwa ukweli uwekea neema ya kuokoa kwa yule anayebatizwa na kumuunganisha na mwili wa Kiroho wa Kristo. Hilo tendo la ubatizo hufanya kazi kivyake, kwa hivyo yule mtoto mchanga anayebatizwa hafai kuwa na imani yeyote wala kupeana idhini ndipo ubatizwe. Lakini haya maelezo ya ubatizo haiambatani na injili. Kuunganishwa na Kristo kwa imani ndiyo njia ya pekee ya wokovu na wala si kubatizwa. Kanuni ya ubatizo na meza ya Bwana, inaonyesha kwamba muungano huo ulifanyika tayari. Ubatizo na meza ya Bwana si msingi wa kuunganishwa na Kristo.

Kuna makanisa mengine ambayo hushikilia kuwa wale watoto wachanga wanaobatizwa wako na imani. Lakini kwa nini wengi wa wale wanaobatizwa wakiwa watoto wachanga hawaonyeshi ishara ya imani kamwe? Imani yao ilienda wapi?

Makanisa mengine ambayo majadiliano yao msingi wake ni Agano za Mungu na ishara za agano hizi. Agano ni husiano ambayo mungu huingia na watu ambao Mungu huthibitisha na kiapo. Agano mara nyingi huja na ishara ambazo zinaonyesha sheria na manufaa ya Agano. Agano la Mungu na Abrahamu ilikuwa na ishiara ya tohara, ambao iliendelea katika Agano la Musa (Mwanzo 17:1;

Mambo ya Malawi12:3). Mungu alifanya Agano na Abrahamu na akamwagiza awafanyie tohara watoto wote wa kiume kama ishara ya Agano.

Makanisa mengine wao huona Matendo 2:38-39 inaeleza kanuni ambayo ilikuwepo wakati wa Abrahamu na inaendelezwa katika Agano Jipya. Wanathibitisha, vizuri, ya kwamba Mungu ana mpango moja ya wokovu ambao anatekeleza kila wakati, na kwamba wale wote watapokea huu wokovu ni watu wake wa ukweli. Pia wanasema ya kuwa kuna  agano moja la neema ambalo wakristo wote katika historia hushiriki. Hii agano hupatikana mara ya kwanza katika ahadi ya mungu kwa Adamu na Hawa katika bustani wa edeni (Mwanzo 3:15), na inatimizwa kwa Kristo. Na kwa ujumla wanasema kwaba kila Agano la Mungu na watu wake ni dhihirisho au utawala wa hii angano moja ya neema.

Kwa hivyo wale ambao wanaoamini kubatizwa kwa watoto wachanga, huona maandashi kama ya Matendo ya Mitume 2:28-39 kama yanaonyesha Agano la Abrahamu na agano jipya pamoja. Baada ya kuwahimiza wasikilizaji wake kutubu na kubatizwa, Petro anasema “Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu na watoto wenu, na kwa wote walio mbali, na kila mtu ambaye Bwana Mungu wetu

atamwita amjie”(Kifungu cha 39). Wale wanaoamini kubatizwa kwa watoto wachanga wanasema ya kwamba, vile Mungu alipanua agano lake na Abrahamu (na kwa hivyo ishara ya agano) kwa watu wake na watoto wao wachanga, hivyo pia anapanua ahadi ya agano jipya (kwa hivyo ishara mpya ya Agano la ubatizo) kwa wakristo na watoto wao. Mwandishi B.B. Warfield alisema hivi kuhusu ubatizo wa watoto, “Mungu aliimarisha kanisa lake wakati wa Abrahamu na akaweka watoto ndani yake, wanastahili kubaki hapo mpaka Mungu awaweke nje. Hakuna mahali Mungu amewaweka nje. Kwa hivyo bado ni wanachama wa kanisa lake na kwa hivyo wako na haki ya kushiriki kanuni zake.”

**Ubatizo wa watoto wachanga si jambo ambalo Biblia inafundisha**

Nina heshima kubwa na upendo kwa wale wakristo wanaounga mkono ubatizo wa watoto wachanga. Wengine wao ni marifiki zangu au mashujaa katika historia. Na hoja ambazo nimezitaja hapo juu zinaonyesha uangalifu kubwa wa neno na heshima ya neno. Lakini sifikiri kuwa zina ushawishi. Hapa kuna sababu sita kwa nini nafikiria hivyo.

1. *Ubatizo wa watoto wachanga inaweka ishara ya muungano na Kristo kwa wale ambao bado hawajaunganiswa na Kristo. Inatoa ishara kutoka kwa ukweli.*

Ubatizo ni muungano wa mkristo na Kristo katika kifo chake, kuzikwa, na ufufuo (Warumi 6:1-4; Wakolosai 2:11-12). Lakini watoto wachanga hawajaunganishwa na Kristo. Watu wote, hata wale wamezaliwa na wazazi wakristo, lazima wampoke Kristo kwa imani ndipo waunganishwe naye kwa njia ya Roho Mtakatiofu.

Watoto wengine ambao wamelelewa katika nyumba za wakristo, hawawezi kukumbuka ni wakati ngani hawakuwa wamemwamini Kristo Yesu. Lakini hii haimanishi kwamba walizaliwa wakiwa wameokoka. Roho mtakatifu lazima awapee imani na toba ya dhambi. Lazima watolewe kutoka utawala wa shetani na kuwekwa katika utawala ya Mwana wa Mungu (Wakolosai 1:13). Lazima wangefufuliwa kutoka kwa kifo, kuokolewa kutoka kwa mkuu wa hii dunia, na kuokolewa kutoka kwa hukumu wa Mungu (Waefeso 2:1-3).

Ubatizo wa watoto unatumia ishara ambayo imetengewa tu wale ambao wameokoka. Huwa inafanya ishara hiyo

ambayo ni ubatizo ikose kuwa na maana yoyote katika maisha ya watoto ambao wanabatizwa. Yule ambaye ameokoka anabatizwa, huwa anatangaza kwamba ameamini injili ya Kristo, na kuna mabadiliko ambayo yamekuja katika moyo na maisha yake. Mabadiliko haya ni, maisha mapya, msamaha wa dhambi, kuoshwa dhambi, kupatanishwa na Mungu, kuzaliwa mara ya pili, na kuwepo kwa Roho Matakatifu katika maisha yake.

Ubatizo wa watoto huwa unatumia ishara ambayo imekusdudiwa kuonyesha haya. Mtoto anapobatizwa na hajaokoka, hiyo ni kazi ya bure kwa kuwa ubatizo si njia ya wokovu, yeye anabaki tu mwenye dhambi kama wenye dhambi wote ambao hawajaokoka. Kwa sababu makanisa hayafai kubatiza watoto ambao hawajaokoka.

*2. Ubatizo wa watoto wachanga huchanganisha kuzaliwa na wazazi wakrisito na kuzaliwa tena kwa nguvu za Roho Mtakatifu.*

Njia nyingine ni kwamba ubatizo wa watoto wachanga huchanganisha kuzaliwa na wazazi wakrisito na kuzaliwa tena kwa nguvu za Roho Mtakatifu. Sisemi kwamba wale wakristo wote wanoamini kubatizwa kwa watoto wachanga huchanganisha haya mambo kwa akili zao.

Mkristo ambaye anaamini kubatizwa kwa watoto wachanga anaweza kuwa anajua ya kwamba mtoto wake mchanga anatakikana kuja kwa Kristo kwa imani dipo azaliwe mara ya pili na Roho Mtakatifu, lakini kwa kumbatiza, tendol enyewe inadhihirisha ya kuwa huyo mtoto amezaliwa mara ya pili na oho Mtakatifu.

Nukuu kutoka kwa "Westminster confession" inasema kwamba ufanisi wa ubatizo haijashikaniswa na wakati ambapo ubatizo unafanyika. Kwa maneno mengine, ubatizo wa mtoto mchanga ingali halali hata kama yule aliiupokea atakuja kumkristo Kristo miakanyingi zijazo. Lakini shida ni kuwa, ishiara enyewe huonge na kusema, "Huyu ameunganiswa na Kristo. Huyu amezikwa na kufufuliwa na Kristo. Huyu amepita kutoka kifo na kuingia kwa maisha mapya katika Kristo." Kama wale wanaoamini ubatizo wa watoto wachanga wanataka ishara ambayo itaonyesha muungano ujao na Kristo, itawabidi watafute kitu kingine lakini siyo ubatizo.

Kwa hivyo ubatizo wa watoto wachanga inapeana ujumbe inayosema kuwa kuzaliwa upya ni kitu ambacho unarithi kutoka kwa wazazi wako. Inaonyesha ya kuwa watoto wachanga wa wakristo wako tofauti kiroho na wale watoto wa wale ambao hawajaokoka wengine. Kwa

hakika watoto wa wakristo wako katika mazigira ya kiroho tofauti kuliko wale watoto wa watu wasiamini. Lakini ubatizo wa watoto wachanga inasema kuwa, tofauti si tu kwa mazigira, bali watoto wenyewe wako tofauti kiroho. Kwa sababu ubatizo ni jambo ambalo linatangaza kile ambacho kimefanyika kiroho katika maisha ya mtu, hatuwezi kamwe kuwabatiza watoto ambao hawajabadilishwa na Yesu Kristo mwenyewe. Kuzaliwa katika jamii ya watu ambao wameokoka, hamfanyi mtoto kuwa amaoekoka, kwani wkovu si wa kurithi, bali imani katika Kristo. Wokovu pia hauji kwa kubatizwa bali kwa kuamini katika Kristo.

*3.Ubatizo wa watoto unaonyesha kana kwamba Mungu analeta watu wake wa agano jipya pamoja jinsi alivyowaleta watu wake pamoja katika Agano la Kale*

Ubatizo wa watoto wachanga inadhania  kwa kimakosa kuwa, kwa njia moja muhimu, Mungu anaumba watu wake wa Agano Jipya jinsi aliumba watu wake wa Agano la Kale. Katika Agano la Kale, Mungu aliwaleta watu wake kwa kuwaweka katika familia na kuwaweka katika makabila tofauti tofauti. Katika Agano Jipya, Mungu anawaleta watu wake kupitia kwa neno lake na Roho

Mtakatifu na kuwaweka ndani ya watu wanoiwta kwa jina lake na anawakusanya kutoka mataifa yote.

Kumbuka kwamba hoja kuu ya wale wanaamini ubatizo wa watoto wachanga inatoka kwa kufananisha ubatizo na tohara. Mungu alimwamuru Abrahamu kupasha tohara watoto wake, dipo watoto wa Abrahamu wakuwe kabila inayotabulika, na iliyo tofauti na wengine waliowazigira. Hili lilifanyika wakati Mungu aliwatoa Waisraeli kutoka Misri na wakati aliwapatia Agano la Musa walipokuwa mlima Siani (2 Wakorintho 3:14). Mungu alipowaita Waisiraeli kutoka Misri, na akawaleta, aliwapa majukumu ya kipekee. Wao walihitajika kutii sharia yake kwa sababu wao walikuwa mali yake. Pia walihitajika kuwa ufalme wa wakuhani na taifa takatifu (Kutoka 19:4-6).

Mungu aliweka wana wa Isiraeli pahali ambapo dunia zima inaweza waona kwa ajili ya kuonyesha mataifa jinsi alivyo. Alitaka wana wana wa Isiraeli watembe katika njia zake kwa sababu ya kufanya mataifa mengine wafuate hizo njia (Kumbukumbu la Torati 4:1-8). Na alitofautisha taifa ya Israeli na mataifa mengine, kwanza kabisa, kwa kuwapasha tohara. Watoto wote wakiume katika taifa la Israeli walifanyiwa tohara (Mwanzo 17:12), na wale wangeni ambao wangetaka kuungana na taifa ya

Isiraeli lazima wangepaswa tohara (Kutoka12:48). Kutoka kwa mwito wa Abrahamu mpaka kuja kwa Kristo, tohara ilikuwa inatofautisha watu wa Mungu na dunia.

Mungu aliwakomboa Waisraeli kujidhihirisha kwa mataifa mengine Yeye ni Mungu wa aina gani. Mungu alitaka Isreali waenende katika njia zake ili mataifa yaliyowazingira waone na wamsifu Mungu (Kumbukumbu la Torati 4:1-8). Yeye aliwatenga Waisraeli kutoka kwa mataifa mengine kwa ishara ya tohara. Wazao wa kiume wa Isreali walitahiriwa (Mwanzo 17:12), na wengine wote ambao walitaka kuungana na Israeli wote walihitajika watahiriwe (Kutoka 12:48). Kutoka kwa kuitwa kwa Abrahamu, hadi kuja kwa Yesu Kristo, watu wa Mungu walijitambusha na kutahiriwa.

Wakati huo wowote, Yule ambaye alikuwa ametahiriwa alikuwa mmoja wa jamii ya Israeli, hata hali yake ya kiroho haikuambatana na kutahiriwa kwake. Kutahiriwa kulidhihirisha kwamba wao walikuwa wa Mungu. Kwa hivyo wale ambao walikuwa wametengwa kuwa watu wa Mungu, walihitaji kuishi maisha ambayo ilidhihirisha kwamba wao walikuwa wa Mungu. “Kwa hiyo tahirini mioyo yenu, na msiwe na shingo ngumu tena”

(Kubukumbu la Torati 10:16; cf  Yeremai 4:4). Lakini, bila shaka, siyo kila mtu aliyepaswa tohara kimwili walikuwa wamepaswa tohara kiroho. Ukiangalia historia ya Wanaisraeli inaonyesha kuwa watu wa mungu waliokuwa katika Agano la Kale hawakumutii Mungu. Waliabudu sanamu, wakanyimana haki na wakafanya uasherati. Wafalme, wakubwa, manabii, Makuhani wao pamoja na watu wote walimugeuka Mungu na wakamukashirisha (Yeremai 32:30-33). Uovu wa watu iliogezeka sana mpaka Mungu hatimaye akawafukuza kutoka kwa nchi yao. Kwanza nchi ya Kaskazini, badaye wale wa Kusini (Kumbukubu la Torati 28:15-68; 2 Wafalme 17:6-23; 25:1-21).

Mungu alikuwa na mpango wa kufanya wanaisiraeli waonyeshe utukufu wake kwa mataifa yote. Aliwapa Agano a Kale ndipo wao waweze kumtii na kukua na wawe tofauti na mataifa  mengine, wakitoa ushuhuda ya hekima yake. Lakini mioyo ya watu zilikuwa na uovu. Sheria haingeweza kutoa suluhu ya dhambi zao. Walikuwa na kila kitu cha faida-Sheria, Kuabudu hekaluni, utukufu wa Mungu kuwepo pamoja nao (Warumi 9:4), na lakini hizo vitu zote mwishowe hazikuwa za manufaa kwao. Wengi wa wale walikuwa

katika agano walishidwa kushikilia agano. Hawakutii na wakahukumiwa.

Kile ambacho watu wa Mungu walihitaji, ni mioyo yao ibadilishwe. Na hiyo ndiyo Mungu aliwahidi katika Agano Jipya.

Siku zinakuja," asema Bwana,"nitakapofanya agano jipya na nyumba ya Israeli na nyumba ya Yuda. Halitafanana na agano nililofanya na baba zao wakati nilipowashika mkono kuwaongoza watoke Misri, kwa sababu walivunja agano langu, ijapokuwa nilikuwa mume kwao,"asema Bwana."Hili ndilo agano nitakalofanya na nyumba ya Israeli baada ya siku zile," asema Bwana."Nitaweka sheria yangu katika nia zao, na kuiandika mioyoni mwao. Nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu wangu.Mtu hatamfundisha tena jirani yake, wala mtu kumfundisha ndugu yake akisema, 'Mjue Bwana Mungu,'kwa sababu wote watanijua mimi,tangu aliye mdogo kabisa kwao, hadi aliye mkuu sana," asema Bwana."Kwa sababu nitasamehe uovu wao,wala sitazikumbuka dhambi zao tena." (Yeremia 31:31-34)

Bwana Mungu anatangaza wazi kuwa hili Agano halitakuwa kama lile Agano alikuwa amefanya na Israeli

katika Mlima Sinai baada ya kuwatoa Misiri. Je, litakuwa tofauti kwa njia gani? Je, hili hawatalivunja? (mstari 32).

Kwa nini hawatavunja hii agano? Kwa sababu Mungu ataweka mafundisho yake, sheria yake, ndani yao na ataziadika kwa mioyo yao (mstari wa 33). Sheria ya Mungu haitakuwa nje ya watu, ikisimama juu yao kama amri isiyo na nguvu. Bali,itaishi dani yao, ikiwaongoza kutembea katika njia za Mungu.

Mungu aliwapea ahadi sawa na hiyo ya awali kwa maneno tofauti anaposema, "Nitawapa moyo mmoja na kutenda pamoja, ili kwamba waniche daima kwa mema yao wenyewe na kwa mema ya watoto wao baada yao. Nitafanya nao agano la milele: Kamwe sitaacha kuwatendea mema, nami nitawavuvia kunicha mimi, ili kamwe wasigeukie mbali nami." (Yeremia 32:39-40). Hili Agano Jipya litadumu milele kwa sababu Mungu mwenyewe atawaezesha watu wake kumwogopa na kumtii, kumshika na wasigeuke bali naye tena. Hii ni njia nyingine ya kusema kuwa atapasha tohara mioyo zao, kuwafanyiya kile hawageweza kujifanyia (Kumbukubu la Torati 30;36).

Mungu anapeana ahadi nyingine sawa na hiyo kwa njia ingine anapotagaza katika kitabu cha Eziekeli, “Nitawapa moyo mpya na kuweka roho mpya ndani yenu, nitaondoa ndani yenu moyo wenu wa jiwe na kuwapa moyo wa nyama. Nami nitaweka Roho yangu ndani yenu na kuwafanya ninyi mfuate amri zangu na kuwafanya kuwa waangalifu kuzishika sheria zangu” (Eziekeli 36:26-27). Mungu atawapa watu wake roho mpya na hata kufanya roho wake mtakatifu aishi ndani yao, na matokeo ya kuwa watatii mapenzi yake kwa njia ambayo hawajawai fanya.Sheria kwa mioyo zao, moyo moja na njia moja, mioyo zilizofanyiwa tohara, moyo wa nyama na siyo ya jiwe, Roho wa Mungu ndani yao- Hizi zote ni njia za kusema kwamba katika agano jipya, Watu wa Mungu watamujua Mungu na kumtii Mungu kwa sababu Mungu mwenyewe atwabadilisha kutoka ndani.

Tazama pia ya kwamba katika agano jipya katika kitabu ya Yeremia 31 majirani hataweza kuwambia majirani wao “Jua Mungu”, “kwa sababu wote watanijua mimi, tangu aliye mdogo kabisa kwao, hadi aliye mkuu sana,”asema Bwana” (Kifungu 34). Watu wote wa Mungu watamujua Mungu. Kitu iliyo wazi katika hizi ahadi zote tumeangalia Munga anaweka wazi; Watu wake wote watabadiliswa. Wale wote walio dani ya agano

watatimiza agano. Wale wote ambao wametambulika kama watu wa Mungu kwa hakika wataishi kama watu wa Mungu. Agano hili jipya litaziba pengo au mwanya uliyopo kati ya watu wa Agano, na watu wanaotimiza Agano.

Watu walikata agano ambayo walifanya na Mungu katika Mlima Sinai na waliteseka uhamisiyoni kama zawadi iliyofaa kwa dhambi zao. Lakini katika agano jipya, watu wote wa Mungu - siyo tu wachache- watamujua na kumtumikia Mungu. Watu wote wa Mungu watapata kusamehewa dhambi zao (mstari wa 34). Watu wote wa Mungu kwa hakika watakuwa watu wa Mungu, siyo tu kwa nje, bali kutoka ndani wao pia. Hili ndilo litatofautisha Agano Jipya na lile la Kale na jinsi Mungu alifanya uhusiano na watu wake (mstari wa 31).

Kwa kifo na ufufuo wa Kristo, Mungu sasa amezinduwa agano jipya (Luka 22:20; Waebrania 9:15). Na wakati wa Pentecoste, Mungu alimwaga Roho wake Mtakatifu kwa watu wake kama alivyo kuwa amehadi kupitia kwa manabii (Matendo ya Mitume 2:1-4). Tangu wakati huo, Mungu amekuwa akiwaita watu wa agano Jipya kwake kupitia kwa neno na Roho.

Katika Agano la Kale Mungu alifanya watu wake kuwaonyesha watoto wa Abrahamu kama kabila iliyotofauti. Aliwapa tohara na sheria ili wakuwe tofauti katika ulimwengu. Lakini siyo wale wote walipaswa tohara kimwili ndiyo walipaswa tohara ya kiroho. Siyo wote walio kuwa dani ya agano walifuata agano. Watu wa Mungu walikuwa wanatabulika kwa tohara bila kuchukulia maanani hali yao ya kiroho.

Lakini katika Agano Jipya, Mungu anafanya na kutengeneza watu kuwa wake kwa njia tofauti. Mtu hahesabiwi haki kwa njia ya kuzaliwa katika jamii ya wakristo. Bali  kupitia kwa neno ambalo Roho Mtakatfiu analitumia kuwazaa watu mara ya pili. Roho Mtakatifu huwafanya watubu na kuamini Yesu Kristo ambaye ndiye njia ya pekee ya kuwa mmoja wa jamii ya Mungu.

Wanao wabatiza watoto, hudhani kwamba Mungu anafanya watu wa Agano kama aliwafanya watu wa wa Agano la Kale. Wale wanaoamini ubatizo wa watoto wachanga huweka watoto wachanga ishiara ya Agano la ubatizo kwa watoto wachanga kwa sababu wanaamini kwaba hawa watoto wachanga wamejumuisha katika agano jipya. Lakini mtu huingia kwa agano jipya siyo kwa uzao wa asili, bali kwa kuzaliwa tena kiroho. Wale

wote waliyo katika agano jipya, dhambi zao zimesamehewa na wanamujua Mungu. Wale wote walio katika Agano Jipya sheria imeadikwa ndani mwa roho zao. Wale wote wako kwa agano jipya roho wa Mungu inaishi ndani mwao, ikiwafanya upya, ikiwawezesha kutembea kwa njia Zake. Kuzaliwa na wazazi wakristo siyo kibali cha kuwa mmoja wa jamii ya Mungu.

Agano jipya haifanyi kazi kwa kuzaliwa bali kwa kuzaliwa tena. Kwa hivyo ishara ya Agano Jipya inafaa kupewa tu wale ambao wana ushahidi wa kuzaliwa mara ya pili kwa kukiri imani yao kwa Kristo.

*4. Ubatizo wa watoto wachanga hutatiza ushuhuda wa kanisa (Mathayo 5:13-16)*

Agano la Kale la Mungu, kwa kubuni, watu walikuwa wamechanganyikiwa kiroho. Ishara ya kimwili ya ubatizo ilikuja kabla, na bila hakikisho ya, ukweli wa kiroho ya roho iliyo pashwa tohara. Lakini hili ndilo jambo haswa Mungu alibadilisha katika Agano Jipya. Kwa kuwafanya watu wa Agano Jipya wote wamebadilishwa, wote wamesamehewa, wote wako na Roho Mtakatifu ndani mwao.

Mara nyingi watu ambao hawajaokoka, hujiunga na kanisa. Lakini hiyo siyo kwa kubuni! Hiyo ni kama kusema kwamba watu wengine ambao wameoana huwa na tamaa na kuzini. Ndiyo, wanafanya, lakini hawafai kufanya! Hiyo ndiyo sababu Yesu alianzisha nidhamu ya kanisa (Mathayo 18:15-20). Wale ambao maisha yao haionyeshi kutubu dhambi siyo washirika wa Agano Jipya na wanapaswa kutengwa kutoka kwa jumuia ya agano jipya. Kwa sababu Yesu aliamuru haya inaonyesha ya kuwa kanisa, tofauti na Isiraeli chini ya agano jipya, inatakikana kuwa jumuiya ya watu ambao wanamujua Mungu.

Ubatizo wa watoto wachanga huwadanganya watu kwamba watajiunga na jumuiya ya watu wa Agano Jipya, ilhali hawajajumuika katika ukweli ya Agano Jipya. Ubatizo huwa huwapotosha watoto kwamba wanaletwa katika kanisa kabla hawajamwamini Kristo kwa mioyo yao. Ubatizo wa watoto unawafanya watu wawe washirika wa kanisa, wao ambao hawajaokoka. Bila shaka, hii itadhuru ushuhuda wa kanisa. Ni jambo la kusitikisha sana kuondoa kanisani mtu ambaye alibatizwa akiwa mtoto mchanga lakini sasa anatenda dhambi bila kutubu kuliko. Ingekuwa vyema kungojea kubatiza kijana mpaka akiri kwa uhakika imani yake kwa Kristo.

Kwa hivyo, licha ya nia mzuri ya wale wakristo ambao hubatiza watoto wachanga, kubatiza watoto itafanya chumvi ya kanisa ikose ladha, na mwagaza wake kutowaka vizuri (Mathayo 5:13-16). Ubatizo wa watoto baada ya muda itafanya kanisa ikae kama dunia, kwa sababu inaleta dunia kanisani.

*5. Ubatizo wa watoto wachanga huondoa tofauti muhimu kati ya ubatizo na tohara*

Ubatizo wa watoto wachanga hutoa tofauti mbili muhimu kati ya ubatizo na tohara. Kwanza kazi ya tohara ilikuwa kuweka alama watu wa Mungu kama kabila iliyo tofauti. Tohara ilikamilisha hii kazi hata kama roho ya mtu haikuwa imepaswa tohara.  Tohara ilikuwa moja wapo ya njia ambazo Mungu alitumia kufanya watu wake wa Agano la Kale kupitia kabila, na familia. Mara nyingine wale wanao unga mkono ubatizo wa watoto wachanga huzuingatia vifungu vya tohara hadi wansahau kuangalia kazi yake ya tofautisha watu kwa kabila na historia. Ubatizo kwa upande mwingine huonyesha njia nyingine ya asili: kuzaliwa na Roho Mtakatifu.

Ya pili, tohara iliweka alama kwa wanaisaraeli kuonyesha kuwa walikuwa watu wa Mungu. Ili takasa mtu kwa Mungu, kumuigiza katika “utakatifu” wa Mungu-hiyo ni, taifa ilichaguliwa. Kwa hivyo, tohara ilikuwa inaonyesha haja ya watu wa Mungu kutakasa mioyo na maisha yao ili waweze kuishi maisha inaolingana na agano. Watu wangu wa Israeli walikuwa wamesha paswa tohara lakini Mungu wapashe tohara mioyo zao (Kumbukubu la Torati 10:16; Jeremia 4:4). Na hilo tendo la kukataa sehemu ya mwili ya mwanaume inaonyesha kuwa mtu atateska- kukatwa katika uwepo wa Mungu na watu kama hangetii agano (Mwanzo 17:11-14). Kwa maneno mengine, tohara inahitaji utakatifu. Ili kuwa inaonyesha jinsi wanaisraeli walihitaji asili mpya.

Ubatizo, kwa upande mwigine, inathibitisha ya kuwa mtu amezaliwa tena, amekuwa mpya, amefanywa upya na Roho Mtakatifu. Ubatizo inathibitisha ya kuwa mtu ameungana na Kristo na yuko na maisha mapya ndani yake. Agano Jipya halimrishi wakristo, “Kwa hiyo tahirini mioyo yenu, na msiwe na shingo ngumu tena” (Kumbukumbu la Torati 10:16). Badala yake, linaamuru wakristo “Au hamjui ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Kwa hiyo tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti,

ili kama vile Kristo alivyofufuliwa kutoka kwa wafu kwa utukufu wa Baba, vivyo hivyo sisi nasi pia tupate kuenenda katika upya wa uzima" (cf. Warumi 6:1-4). Ubatizo inaashiria ahadi ya maisha mpya inaopatikana kwa Kristo katika maisha ya mkristo. Tohari ilimfanya mtu awe na hali ya kutakasika na kuhitaji mtu atakase moyo wake; ubatizo inasema moyo ishatakaswa katika Kristo.

Wale wanaamini katika ubatizo wa watoto wachanga wanachora mstari sawa kutoka tohara hadi kwa ubatizo.Tohara ya kimwili inapata kutimizwa katika agano jipya kwa ubatizo. Lakini hiyo siyo mstari mtume Paulo anachora. Fikiria kuhusu Wakolosai 2:11-12:

Katika Kristo pia mlitahiriwa kwa kutengwa mbali na asili ya dhambi, si kwa tohara inayofanywa kwa mikono ya wanadamu, bali kwa ile tohara iliyofanywa na Kristo, mkiwa mmezikwa pamoja naye katika ubatizo, na kufufuliwa pamoja naye kwa njia ya imani yenu katika uweza wa Mungu, aliyemfufua kutoka kwa wafu.

Paulo anasema kuwa wakristo wanatakiwa kufanya tohara. Je, hili linafanyaika kwa njia gani? Ilikuwa tohara iliofanywa "bila mikono" hiyo nikusema, haikufanywa na

mwanadamu yeyote. Nani sasa alitufanyia tohara? Ilifanyika wakati tuli "weka kando mambo ya kimwili" wakati tulitupilia bali asili yetu ya Kale, ya dhambi. Nani yuko na nguvu ya kufanya hivyo? Bila shaka ni Mungu tu. Kwa hivyo sisi wakristo "tulipaswa tohara" wakati Mungu mwenyewe alitupulia bali hali yetu ya Kale, akauwa asili yetu ya dhambi, na akatupatia moyo mpya, Roho mpya, mtu mpya katika Yesu. Kwa maneno mengine, Paulo anasema kwamba wakristo wote wame kuwa kwa hali ya tohara ya moyo ambayo Mungu alihitaji wana israeli wafanye na alikuwa amehadi kupitia kwa manabii.

Hii iko na uhusiano upi na ubatizo? Paulo anasema hapa ya kwamba katika ubatizo,tulizikwa na kufufuliwa na Yesu kupitia imani. Kwa sababu ubatizo ni mahali abapo imani hujitagaza, Paulo anatumia ubatizo kama kumbukumbu ya hali yetu yote ya kubadilishwa. Tuliweka kado asili yetu ya Kale wakati gani? Wakati tulizikwa na kufufuliwa na Kristo kupitia imani. Ubatizo unaonyesha kifo na ufufuo pamoja na Kristo kwa imani.

Kwa hivyo tohara iko na uhusiano upi na ubatizo? Ubatizo ni alama ya agano jipya ya kutahiri moyo siyo mwili. Ubatizo inaashiria hali halisi, ambayo tohara

ilikuwa inahitaji lakini haikuweza kudhamini, na sasa imekuwa ukweli katika maisha ya Mkristo. Ubatizo inasema ya kwaba ile ambayo tohara ilikuwa inaonyesha kwa ubali lakini haikuwa nao imefanyika sasa. Tohara imetimizwaje katika agano jipya? Siyo kwa kubatiza watoto wachanga, ambao bado- na huenda kamwe hataweza- kuwa katika hali halisi ya agano jipya. Badala yake, tohara inatimizwa katika agano jipya kwa njia ambayo ubatizo inaonyesha tohara ya moyo. Tohari ilisema kwa wana wa Israeli, “Jifanye upya! ” Ubatizo inasema kwa wakristo, “Huyu amefanywa upya!”

6. *Ubatizo wa watoto wachanga unafanya Agano Jipya la Mungu kuwa ahadi isiyo kamili*

Mwishowe, ubatizo wa watoto wachanga inafanya Agano Jipya la Mungu kuwa ahadi isiyo ahadi kamili. Wale wanaoamini ubatizo wa watoto wachanga huwa na uzoefu wa kunukuu Matendo ya Mitume 2:38-39, ”Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu na watoto wenu.” Lakini sasa tunaogea juu ya ahadi gani hapa? Wale wanaoamini ubatizo wa watoto wachanga wanasema ya kwaba Munga anafanya ahadi ya agano jipya kwa wakristo pamoja na watoto wao. Na bado wanakubali kuwa wengi wa wale ambao wanabatizwa wakiwa watoto wachanga huwa

hawaji kwa Kristo. Wengi wa wale ambao hupokea ishiara ya agano jipya wakiwa watoto wachanga hawatawai kuwa katika hali halisi ya agano jipya. Kwa maana gani, basi, ndiyo ahadi ya Mungu ya agano jipya huwa ahadi kwa kweli?

Nitasema ya kwamba, kulingana na mazoea ya wale wanaoamini ubatizo wa watoto wachanga, kwao siyo ahadi. Kwa kupuguza hii shindikizo, wengi wa wakristo wa wanaoamini ubatizo wa watoto, kwa njia moja au nyigine husema ya kwamba kuna njia mbili ya kuwa wa agano jipya- moja ya nje, moja ya ndani. Kwa maneno mengine, unaweza kuwa mmoja wa Agano Jipya na dhambi zakoziwe  hazijasamehewa, na moyo wako usiwe umeadikwa sheria ya Mungu, na usiwe unajua Bwana. Lakini kama tushaona hii mgawanyiko kati ya kukuwa kwa agano na kutimiza agano ndiyo kitu hasa agano jipya la Mungu ina ahidi kufuta. Katika agano jipya Munga ana ahidi kuwa wale wote watakuwa kwa agano watatimiza agano na watakuwa na uzoefu wa baraka, kwa sababu Mungu mwenyewe atadhamini wafanye hivyo. Mungu mwenyewe ataandika sheria zake kwa mioyo yao, na kuwapa ujuzi  wa Ukweli, nakuwasamehe dhambi zao (Jeremia 31:31-34). Sababu nzima ya agano jipya ni kwamba kukua katika Agano, ni kutimiza agano; kukuwa

katika agano jipya, ni kukuwa na moyo mpya; nafsi mpya.

Kwa kuwafanya watoto wachanga wa wakristo katika agano jipya, wale wanaoamini ubatizo wa watoto wachanga hufanya ahadi ya Mungu ya agano jipya kuwa ahadi isiyo halisi. Ubatizo wa watoto wachanga inarudisha nyuma maendeleo ya historia ya wokovu na kuingiza kwa agano jipya mgawanyiko ambayo Mungu aliharibu- pengo kati ya kukuwa katika Agano na kutimiza Agano, kukuwa sehemu ya watu wa Mungu na kumujua Mungu kwa Ukweli.
Ubatizo wa watoto wachanga inabuni kikundi “katika agano jipya, lakini siyo wa agano jipya.” Inafanya ahadi ya Mungu kukuwa ahadi isiyo kamili. Ubatizo wa watoto wachanga siyo dhamana kuwa huyo mtoto atakuwa akimjua Bwana, vile wanaoamini ubatizo wa watoto hukubali. Lakini basi ni “ahadi” gani anafanya kwa watoto wa wakristo? Siyo ahadi ya agano jipya. Siyo ahadi ya Mungu kama kama inaweza kuwa haitatimizwa.

**Kujibu pingamizi ya wale wanaoamini katika ubatizo wa watoto wachanga.**

Kwa hakika, wale wanaoamini ubatizo wa watoto wachanga hutoa pingamizi kwa hoja ambazo nimezitaja hapo. Kwa ajili ya usahihi na haki, hebu tuzijadili taratibu pingamizi hizi tano.

*1.Ubatizo katika kitabu cha Matendo ya Mitume unaonyesha kuwa katika agano jipya Mungu bado anashugulika na watu wake kama familia miongoni mwa familia nyingi.*

Wale wanaoamini ubatizo wa watoto wachanga mara nyingi huonyesha ile inaitwa “ubatizo ambao ni wa jamii yote” ya Matendo ya Mitume( kwa mfano, Matendo ya Mitume 16:15, 31-34; cf 1 Wakorintho 1:16) kuonyesha kuwa katika agano jipya Mungu bado anashugulika na familia kama familia. Kama kaya mzima inaweza batizwa wakati kichwa ya familia aliamini, basi kwa hakika hiyo lazima imejuisha watoto wachanga. Na hata siyo hivyo, inaonyesha ya kuwa wokovu wa Mungu anafanya kazi kupitia familia, siyo kando na hao, kwa hivyo ubatizo unafaa kupeanwa kwa watoto wa wakristo.

Hivyo ndivyo hoja inaendelea. Lakini maadhishi yanasema nini kuhusiana na kweli? Hapa kuna maelezo

ya  Paulo na Sila pamoja na mfanyakazi wa jela kutoka mji wa Filipi.

Wakamwambia neno la Bwana yeye pamoja na wote waliokuwako nyumbani mwake. Wakati ule ule, yule mkuu wa gereza akawachukua, akawaosha majeraha yao, kisha akabatizwa yeye pamoja na wote waliokuwa nyumbani mwake bila kuchelewa. Akawapandisha nyumbani mwake akawaandalia chakula, yeye pamoja na nyumba yake yote wakafurahi sana kwa kuwa sasa walikuwa wamemkristo Mungu. (Matendo ya Mitume 16:32-34)

Kwanza, tambua ya kwamba Paulo na Sila "Wakamwambia neno la Bwana" kwa kila mtu aliyekuwa kwa nyumba. Yeyote aliyekuwa katika nyumba alikuwa mzee kiasi cha kuweza kuhubiriwa injili. Hii ni dhahiri kwamba hakukuwa na watoto. Ya pili mkuu wa gereza alifurahi alipomwamini Mungu "pamoja na wote waliokuwako nyumbani mwake" . Neno la kigiriki hapa " na wote waliokuwako nyubani mwake" inaweza elezea kufurahia au kuamini, lakini maana ya sentensi inaitaji zote. Watu waliokuwako katika nyumba ya mkuu wa gereza walifurahi pamoja naye kwa sababu wao, kama yeye, walisikia injili, wakaamini, nawakabatizwa.

hizi vifungu kwa namna yeyote hazitenganishi  ubatizo na kuamini injili. Hazipeani nafasi ya kupanua ishara ya injili kwa wale ambao hawajaamini injili. Na maelezo mafupi katika Matendo 16:15 inafaa kusomwa ikizigatiwa maelezo zaidi hapa. Zaidi, kama hivi vifungu vinatufundisha kubatiza watu wa mayumba ambao hawajamwamini Kristo, kwa nini wale wanaounga mkono ubatizo wa watoto wachanga hawabatizi wale ambao wameoana, hata kama hajakuja kwa imani? Na vijana wao je au watoto wao wazima?

*2. Paulo anawabia watoto  watii wazazi wao “ katika Bwana” (Waefeso 6:1) na anawaita watoto wa wazazi wakristo “watakatifu” (1 Wakorintho 7:14). Hii inadhania kuwa watoto hao ni wa agano.*

Katika Waefeso 6:1 Paulo anawambia watoto watii wazazi wao “Katika bwana”, na Katika 1 Wakorintho 7:14  anasema kuwa watoto wa wakristo ni “watakatifu”, hata kama mzazi mmoja siyo Mkristo. Hii haionyeshi kuwa Paulo anaona watoto kama wanachama wa agano jipya?

Acha tuanze na Waefeso 6:1.  Inamaanisha nini Paulo akiwazungumzia hawa watoto kama wale walio “katika Bwana”? Nafikiri Msomi wa agano Jipya wa Presbyterian Frank Thielman anapeana jibi mzuri. Katika Waefeso yote haya maneno inahusu wakristo kuunganiswa na Kristo. Wakristo ni hekalu takatifu “katika Bwana” (2:21), Wakristo walio Efeso walikuwa kwa giza zamani lakini sasa wamekuja kwenye nuru “katika bwana” (5:8), na kuendelea (cf. 4:1, 17). Kwa nini sasa Paulo anaogea na watoto jinsi hii? “Kwa sababbu wame igizwa ndani ya Kristo kwa imani (1:13), wanastahili kutii wazazi wao.”

Kwa maneno mengine, Paulo hazungumzii watoto kama wana agano jipya ambao labda au labda hutuunganisha na Kristo kwa imani. Badala yake, anazungumza na watoto kama wakristo, na anawambia watii wazazi wao kama wakristo. Hashughuliki  swali ya kama yule mtoto wa wakristo ambaye haamini wako na hali maalum ya agano.

Katika 1 Wakorintho 7:14, Paulu ana sahihisha mawazo mabaya kwamba ikiwa mtu yuko katika ndoa, na aokoke anapaswa kuachana na Yule mwingine ikiwa hajaokoka. Anasema, “Kama huyo mume asiyeamini anatakaswa kupitia mkewe, naye mke asiyeamini anatakaswa kupitia mumewe. Kama asingalikuwa hivyo, watoto wenu

wangalikuwa si wasafi, lakini hivyo ilivyo sasa wao ni watakatifu." Wale ambao wanabatiza watoto wao huwaza kwamba Paulo anamaanisha kwamba watoto wa wale ambao wameokoka ni watakatifu kwa sababu wao ni washirika wa Agano Jipya hata wao kwa kweli hawajapokea ahadi za Agano Jipya.

Kitu cha kwanza cha kukumbuka hapa ni kuwa maandiko hayasemi kitu chochote wazi kuhusu ubatizo. Cha pili, Paulo anaeleza kuwa yule mke au mume ambaye haamini kuwa "mtakatifu" kwa njia moja kama watoto. Kwa hivyo, hoja yeyote hapa kuhusu ubatizo wa watoto wachanga inafaa pia kuwa hoja kwa ubatizo wa watu wazima ambao hawajamini! Ni watu wachache sana wanaoamini ubatizo wa watoto wachanga huchukua hiyo hatua, kwa hivyo hii hoja kutoka kwa hii kifungu haifai.

*3. Katika Warumi 4:11, Paulo anasema kuwa Abrahamu alipokea ishara ya tohara kama muhuri ya haki aliyokuwa nao kwa imani.*

Katika Warumi 4:11 Paulo anasema "Alipewa ishara ya tohara kuwa muhuri wa haki aliyokuwa nayo kwa imani hata alipokuwa bado hajatahiriwa. Kusudi lilikuwa

kumfanya baba wa wote wale waaminio pasipo kutahiriwa na ambao wamehesabiwa haki."

Kwa hivyo Paulo anafundisha kuwa ishara ya tohara ilikuwa, kwa Abrahamu, muhuri ya haki aliyokuwa nao kwa imani kabla hajapaswa tohara. Wanao amini ubatizo wa watoto wachanga wanaashiria kuwa watoto wa Abrahamu, waliopashwa tohara wakiwa miaka nane, walipokea hii "muhuri" ya haki kwa imani hata kabla washiriki imani ya Abrahamu na haki inayotokana na imani. Kwa maneno mengine, Mungu aliamuru Abrahamu kupanua "lengo" ya ishara ya tohara bila kujali kama ukweli wa haki inayotoka kwa imani ilikuweko. Zaidi, wale wanaoamini ubatizo wa watoto wachanga husema kuwa ubatizo na tohara kimsingi zinaishiria ukeli moja: Tohara iliashiria haki kwa imani, na ubatizo inaashiria muungano na kiristo, ambaye tuko na haki kwa imani. Kwa hivyo, kama tu tohara, ubatizo inafaa kufanyiwa watoto wa wana agano kama "lengo" ya ishara ya muungano na Kristo hata kama ukweli wa imani upo ama haupo.

Lakini hii siyo nukuu ambayo Paulo anaifanya katika kifungu hiki. Nukuu ya Paulo ni mpangilio ya haki na tohara: Abrahamu alihesabiwa haki kwa imani kabla

yakupaswa tohara. Mwanzo 15 inatangulia Mwanzo 17. Paulo anafanya hii nukuu kusisitiza ukweli ya kuwa Abrahamu ni “baba wa wote wale waaminio pasipo kutahiriwa na ambao wamehesabiwa haki” Warumi (4:11). Kwa maneno mengine, wale watu wasiyo tahiriwa watakao amini Kristo watatagazwa wa haki kwa imani kama vile Abrahamu alivyo. Hawaitaji tohara diposa wapokee baraka za agano, kwa sababu Abrahamu mwenyewe hakukuwa amepaswa tohara alipopokea haki kwa imani.

Kwa maneno mengine, Paulo anaongea kuhusu tohara ya Abrahamu, siyo ya kila mtu. Anaongea kuhusu  kile inamanisha kwa Mungu kutagaza Abrahamu kuwa wa ahaki kabla kumpatia Agano la tohara. Paulo hafundishi kuwa tohara kwa asili inashiria kupata na haki kwa imani; badala yake, anafudisha ya kuwa ishara ya tohara ilikuwa muhuri  ya haki ya Abrahamu kwa imani. Mungu alimpa Abrahamu tohara kama  thibitisho ya msimamo wa haki alikuwa nayo na Mungu. Nukuu ya Paulo siyo kuhusu kitu ambacho tohara inaashiria kwa wote wanaoipokea, lakini kile Mungu alikuwa anamwabia Abrahamu kwa kumpea tohara.

Hatimaye, kifungu hiki hakitaji mahali popote ambapo tunafaa kulinganisha ubatizo na tohara.

*4. Kukata ubatizo wa watoto wachanga ni kufukuza watoto kanisani.*

Wale wanaoamini ubatizo wa watoto wadogo wanasema ya kuwa Mungu alijumuisha watoto wa wakristo kati ya watu wake katika Agano la Kale, kwa hivyo kukata kubatiza watoto wachanga ni kufukuza watoto nje ya kanisa. Lakini hii inaleta swali ya kanisa ni nini na Mungu hufanya kanisa aje? Kama Munga anafanya kanisa lake kwa kuleta ahadi zake za agano jipya kuwa na athari kwa maisha ya watu, basi watoto wasiyoamini hawako "ndani" ya kanisa-mwili zima ya Kristo, wale wameunganisha na Kristo kwa imani- hata kama tutabatiza au hatutawabatiza. Wale wanaoamini ubatizo wa watoto wachanga wanasema kuwa wale ambao hawabatizi watoto wachanga wameshirikisha watoto ambao wanastahili kuwa ndani na kuwaweka nje, lakini hao wamechukuwa wale ambao wangali nje na kuwaleta ndani.

Bila shaka watoto wa wakristo wanastahili kuwekwa pamoja katika maisha ya kanisa kwa maana ya kuabudu

na kanisa, kufudhishwa na kanisa, na kuwa ndani ya uzoefu zaidi milele ya ushirika na kanisa. Wale wanao amini ubatizo wa watu walio kiri imani pamoja na wale wanaoamini ubatizo wa watoto wachanga huamini kuwa tumeitwa kulea watoto wetu " kwa nidhamu na mafundisho ya Bwana" (Waefeso 6:4). Kufundishwa na kuagizwa kwa Bwana inahushisha kushiriki kwa zaidi katika maisha ya kanisa, kwa njia zinazo faa amri ya mtoto, ukomavu, na hali yake ya kiroho.

*5. Kukata ubatizo wa watoto wachanga ni kuhimiza umoja wa maandiko na mpango wa Mungu wa wokovu.*

Wanoamini ubatizo wa watoto wachanga wanapenda kusisitiza umoja na kuendeleza mpango wa Mungu ya Wokovu. Wanapenda kuangazia yale ambayo yanaonyesha kuendelea kwa mpango huu wa Mungu. Kwa pamoja kila mkristo anafaa kusema "Amina!" Kuna Mungu moja, mpango wake wa wokovu ni mmoja. Anakusanya watuwake wote kutoka mataifa kupitia kwa Kristo na watarithi pamoja naye milele.

Lakini kila Mkristo anafaa kushughulikia kutoendelea kwa mpango wa Mungu ya wokovu. Hatutowi tena dhabihu katika hekalu la Yerusalemu. Sisi si hatu fugwi

na sheria ya Mungu ili kudumisha ibada safi, kujitenga na chakula ilivyohitajika na sheria ya Musa, na kuendelea. Kila Mkristo anafaa kusawazisha vile vitu vinaendelea na vile haviendelei kati ya Agano la Kale na agano jipya. Kama wakristo wengine watasisitiza kuwa wakristo watahiri watoto wao kwa kutii sheria ya Musa, wale wanaoamini ubatizo wa watoto wachanga watajibu aje? Pamoja na Paulo, watasisitiza kuwa wakristo kama hao wanaturudisha nyuma katika historia ya wokovu na kufuta vita ambazo haziendelei kati ya vile Mungu alifanya kazi katika Agano la Kale na agano jipya.

Kila mtu anaona vitu ambavyoo vinaendelea na vile haviendelei kati ya Agano la Kale na agano jipya. Hili ni kupata usawa vizuri. Na ningesema, na nimesema katika sura huu, kubatiza watoto wachanga ni kusisitiza maendeleo mahali ambapo agano jipya enyewe inasisitiza kutoendelea. Kubatiza watoto wachanga ni kuleta kutoka Agano la Kale kwa agano jipya mpangilio ambayo agano jipya inavuja.

## Kubatizwa kwa watoto wachanga ambao hawajaokoka si ubatizo wa kweli

Hii yote inaongeza nini? Ya kuwa ubatizo wa watoto wachanga si kitu abayo biblia inamanisha ubatizo kuwa. Bibilia haiamuru wala kukubali makanisa kubatiza watoto wachanga. Hata kama maoni ya wale wa mrengo wa agano wanao amini ubatizo wa watoto wachanga inapedeza, haingiliani na kile ambacho Maandiko yanafundisha kuhusu ubatizo na agano jipya. Ubatizo wa watoto wachanga siyo ubatizo.

Kwa hivyo kama “ulibatizwa” ukiwa mtoto mchanga, ni tumani yangu kuwa utakuja kuelewa kutoka kwa Biblia kwa nini hiyo “ubatizo” haikuwa ubatizo. Siyo kwamba ubatizo wa watoto uko na uharibifu fulani, kama gari iliyo na kifaa kibaya na bado inaweza kufanya kazi. Badala yake, ubatizo wa watoto wachanga siyo ubatizo hata kidogo. Wale waliobatizwa wakiwa wachanga, hawajabatizwa kwa ukweli, kwa hivyo wanahitaji kubatizwa. Siyo kubatizwa tena, lakini kubatizwa kwa sababu hawajawahi kubatizwa kulingana na mafundisho ya kweli ya Biblia.

Wengine ambao wamekuja kuelewa huu ukweli bado wanasita kubatizwa, ingawa, kwa sababu wanaona kubatizwa kama kupinga wazazi wao-au angalau, wanaogopa kuwa wazazi wao wataiona ikiwa hivyo. Kwa hakika tunafaa kuheshimu wazazi wetu na kuonyesha kwa upole na heshima tofauti yoyote ya theolojia ambayo tuko nayo. Kama Yesu anaelewa ubatizo tofauti na vile wazazi wetu wanaelewa, basi ni Yesu tunafaaa kumtii badala ya wazazi wetu (Luka 14:26).

## Kwa nini Ubatizo unahitajika ndipo mtu awe mshirika wa kanisa?

Wengine wenu mnasoma hiki kitabu kwa sababu unataka kujiunga na kanisa na unahitajika ubatizwe ndipo ujiunge. Lakini kwa nini makanisa yanahitaji ubatizo ndipo mtu afanywe mshirika wa kanisa? Hiyo ni mazoea ya biblia kweli? Hiyo haitatenga wakristo wengine wa kweli kwa kufanya washirikas, kwa kuwa siyo wakristo wote hukubaliana na nini inafaa kuwa ubatizo?

Hii sura inajibu haya maswali yote kwa kuonyesha funzo la biblia kuhusu ni kwa nini ubatizo unahitajika ili mtu awe mshirika wa kanisa. Kwa uwazi, nikesema “ubatizo”, ninamaanisha ubatizo wa wakristo, siyo watoto wachanga. Kama vile tulivyoona katika sura iliopita, “ubatizo” wa watoto wachanga siyo ubatizo.

Hii sura pia imeadikiwa viogozi wa kanisa, wale ambao wako na ushawishi. Kama kanisa yao itahitaji ubatizo ndipo mtu akuwe mshirika wa kanisa. Nia yangu ni kukushawishi kuwa unahitaji ubatizo. Nitafanya kesi kwa

hatua saba, halafu nitashugulikia pingamizi iliyo na nguvu.

**Sababu Saba tutazingatia Kwa nini Ubatizo unahitajika ili uwe mshirika wa Kanisa.**

Hakuna maandishi inayopeana ushahidi wa moja kwa moja kwa uhakika kwa hoja hii. Kwa hivyo ili kutambua kwa nini ubatizo unahitajika ili mtu awe mshirika wa kanisa, tunahitaji kupima na kuweka pamoja vifungu vingi vya biblia. Hii sura itakuwa ngumu kiasi kuliko zingine, lakini kile tunasema hapa ni kueleza zaidi ufafanuzi wa maana ya ubatizo ambayo tuliangalia katika sura 1. Hapa kuna sababu saba, ambazo zitazingatiwa kwa pamoja, zitaonyesha kuwa Bibilia inaonyesha ubatizo kuwa kitu cha lazima ndipo mtu awe mshirika wa kanisa.

1. *Ubatizo ni mahali ambapo imani hutagazwa hadharani.*

Kumbukuka maana ya ubatizo tulioweka katika sura ya kwanza: *Ubatizo ni kitendo cha kanisa kuthibithisha na kuonyesha ushirika wa mkristo na Krsito kwa kumzamisha kwenye maji, na pia ni kitendo cha mkristo kudhihirisha hadharani kujitolea kwake kwa Kristo na*

*watu wake, na kwa hivyo kuunganisha mkristo na kanisa na kumtofautisha na dunia.*

Kwa maneno mengine, ubatizo ni mahali ambapo imani hutagazwa hadharani. Maisha ya Mkristo ni maisha ya ushahidi ya mbele ya watu (Mathayo 10:32-33), na hiyo ushahidi huanza wakati wa ubatizo.Wakati wa pentecoste wale watu waliobadilishwa na mahubiri ya Petro walitoka kwa umati, wakitangaza utii wao kwa Kristo kama Bwana na Mwokozi kwa kunyenyekea kwa ubatizo (Matendo2:38-41). Katika ubatizo tunajitoa wenyewe kama wakristo. Tunajionyesha mbele ya watu kuwa tumesulubiwa na kufufuka na Kristo na watu wake.
Kama tulivyo ona, Yesu aliamuru wanafunzi wake kufanya wanafunzi kwa kuwahubiria injili halafu, kuwabatiza, na kuwafundisha kutii kila kitu aliwamuru (Mathayo 28:19). Kwa hivyo siyo kitu cha kushangaza kuwa wakati wa Pentecoste Petro aliamuru wale walikuwa wakimsikiza “Tubuni, mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina la Yesu Kristo, ili mpate kusamehewa dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu” (Matendo 2:38). Kama unahisi kuwa unamfuata Kristo, hii ndiyo amri ya Kristo ya kwanza unafaa kutii. Baada ya kumuamini Kristo, ubatizo ndilo jambo la kwanza mkristo mpya anapaswa kulifanya.

Kama haujabatizwa, bado haujachukua hatua ya kwanza baada ya kuokoka.

Kwa nini ubatizo unahitajika ndipo mtu awe mshirika wa kanisa? Kwa sababu ubatizo ni mahali ambapo imani hutagazwa kwa watu wote. Ni mahali ambapo imani isiyoonekana inaonekana. Ni mahali ambapo mkristo anajitambulisha na kanisa na anasema mimi si wa ulimwengu.

*2. Ubatizo ni kiapo -ishara ya ya kuanzisha agano jipya*

Kwa sababu ubatizo ni njia ambayo mkristo hujitolea mwenyewe kwa Kristo na watu wake, ubatizo pia ni kiapo-ishara ya kuazisha agano jipya. Ni tendo ambalo huanzisha ahadi ya mtu kumkristo Kristo na kuishi maisha ya agano jipya.

Kupitia kwa kifo chake, Yesu alizidua agano jipya ilio ahidiwa, kama vile tulijadili katika sura uliopita (Jeremia 31:31-34; Luka 22:19-20; Waibrania 8:1-13). Agano zote huthibitiswa na kiapo: ahadi mzuri yakujifanyia.Bado kiapo si tu kitu ya kuongea, ni kitu inaweza tendeka, au kuwa katika hali ya kazi. Wakati Mungu alifanya agano na Abrahamu, alipata katikati wanyama waliokuwa

wamekatwa nusu nusu( Mwanzo 15:1-21). Hii kiapo-ishara ilithibitisha ahadi ya Mungu kwa Abrahamu na ikaonyesha kuwa kama Mungu hatakuwa mkristofu kwa Agano lake, yenye mwenyewe ataubeba hukumu. Katika kifo ya Yesu Kristo, Mungu Mwana aliubeba hukumu-siyo kwa kutokuwa mkristofu, lakini kwa sababu ya sisi kutokuwa waaminifu. Agano jipya ilithibitishwa wakati Yesu Mwenyewe alilipa deni ya dhambi zetu (Waebrania 9:15).

Agano la Kale ilikuwa na tohara, ishara yenye ilithibitisha kuingia kwa mtu kwa agano. Kwa hivyo hata agano jipya hukuja na kiapo-ishara -kwa kweli mbili. Ya kwanza, ubatizo ndiyo kiapo-ishara ya kuanzisha agano. Ni picha nadhiri  inaothibithisha kuingia kwa mtu katika agano jipya. Katika ubatizo tunamwoba Mungu atakubali kwa maneno Agano lake Jipya( 1 Petro 3:21), na tunajitolea kutimiza, kwa neema, yote ambayo Agano lake jipya inatuhitaji kufanya (Mathayo 28:19). Katika ubatizo tunaapa nadhiri, “Unamuchukuwa huyu Yesu kuwa Bwana na Mwokozi wako?” “Ndiyo naapa.”

Kwa hivyo wakati kanisa inauliza, “ Ni nani ndiye mtu wa agano jipya?” sehemu moja ya jibu ni, “ni nani ameapa kiapo?” Hiyo ni, nani amebatizwa? Kama tu vile

askari hawezi chukua silaha kabla hajaapa kutii nchi yake, huwezi ingia katika ushirika ya agano jipya mpaka huape kiapo ya agano. Kanisa ni mahali ambapo agano jipya inajionyesha duniani, na ubatizo ni njia ambayo mtu hujionyesha kama mshirika wa agano jipya. Ubatizo ni lazima ili mtu awe mshirika wa kanisa kwa sababu ubatizo ni kiapo-ishara ya kuanzisha agano jipya.

*3. Ubatizo ni pasipoti ya ufalme na sherehe ya ufalme ya kuapishwa mshirika*

Tatu, ubatizo ni pasipoti ya ufalme na sherehe ya ufalme ya kuapishwa raia. Kama vile tulivyoona katika sura 1, wakati Yesu alizindua Ufalme wa mbiguni duniani, aliazisha kanisa kama ubalozi ya hiyo ufalme. Alipeana kwa  kanisa "funguo za ufalme" ili waweze kutambua wananchi mbele ya ulimwengu kwa kuthibitisha ukiiri ya wale wanao kiiri imani yao iliyoaminika kwa kristo (Mathayo 16:19; 18:18-19). Na ile njia ya kuazisha ya kwanza ambayo kanisa hutumia kutabua watu kama wanaichi wa ufalme ni ubatizo (Mathayo 28:19). Ubatizo ni njia ambayo kanisa hutangaza, "Huyu ni wa Yesu."

Ubatizo ni pasipoti ya ufalme. Tunakuwa wananchi wa ufalme kwa kuweka imani yetu ka Mfalme, na katika

ubatizo kanisa hutabua na kutibisha uraia wetu. Na ubatizo huwezesha balozi zingine wa ufalme - kanisa zingine- kututabua kama raia wa ufalme.

Kwa upande mwingine, ubatizo ni sherehe ya ufalme ya kuapisha raia. Ni njia yetu ya kuchukua kirasmi ofisi yetu mpya ya  kuwakilisha Kristo na ufalme wake duniani. Kwa hivyo, ili kanisa iweze kutabua mtu kama raia wa ufalme, huyo raia anafaa kutoa pasipoti yake. Ubatizo unahitajika ndipo mtu awe mshirika wa kanisa kwa sababu ni pasipoti ya ufalme na sherehe ya ufalme ya kuapisha mshirika.

*4. Ubatizo ni njia inayotakikana kwa sababu kanisa humtambua Mkristo.*

Sababu ya nne ya kwa nini ubatizo inahitajika ndiposa mtu awe mshirika wa kanisa ni kile ambacho inamanishwa na hoja tatu za kwanza. Kwa sababu ubatizo ni njia ya kanisa kutambua mbele ya watu mtu kama Mkristo, pia ni njia inayotumika na kanisa kujua Mkristo ni nani. Ubatizo ni kama kitambulisho cha kutambua, na pia ubatizo ni fulana ya timu ya Ukristo.

Kwa hivyo ubatizo ni muhimu, ingawa haitoshi, kutumika na kanisa kama njia ya kutambua Wakristo. Haitoshi tu mtu kudai kuwa yeye ni Mkristo, au kwa kila mtu kanisani kufikiria mtu ni Mkristo; Mungu amefunga hukuma ya kanisa kwa ubatizo. Yesu alitupa ubatizo, kwa sehemu, ili tuweza kujitambua uliwenguni.Kwa kutambua watu kama wakristo mbele ya watu, ubatizo huchora laini kati ya kanisa na ulimwengu. Ubatizo hupeana alama inaotambua Wakristo kama Wakristo, ambayo inamanisha ubatizo ni muhimu kwa mtu kuwa mshirika wa kanisa. Kanisa haijapewa mamulaka ya kumtabua mtu kama mshirika wa timu wa yesu mpaka huo mtu avalie sare ya hiyo timu.

*5.Ubatizo ni ishara ambayo inamfanya mmoja awe na ujasiri wa kuwa mshirika wa kanisa*

Tano, ubatizo ni ishara ambayo inamfanya mmoja awe na ujasiri wa kuwa mshirika wa kanisa. Hii pia inatokana na hoja tatu za kwanza. Kama ubatizo ni mahali ambapo imani inadhihiriswa hadharani, kiapo-ishara ya kuazisha agano jipya, pasipoti ya ufalme, na sherehe ya ufalme ya kuapisha mmoja wao, basi ubatizo ni ishara kamilifu ya kuwa mshirika wa kanisa. Ni ukweli wa kanisa ambalo linaashiria kwamba Mkristo kuwa wa kanisa, na kanisa

kuthibithisha kukiri kwake imani katika Kristo na kumunganisha na kanisa.

Kama kuwa mshirika wa kanisa ni nyumba, ubatizo ni mlango wa mbele. Kwa kuingia kupitia kwa mlango wa mbele unaingia kwa nyumba. Kwa kwaida, kwa hiyo, ubatizo siyo tu kitangulizi ya kuwa mshirika wa kanisa; inapeana fursa ya kuwa mmoja wa kanisa. Ubatizo unakuleta katika ushirika wa kanisa. Kwa mtu mpya ambaye amebadilishwa, ubatizo ni njia ya agano jipya ya kuungana na kanisa. Kwa sababu ubatizo ni ishara halisi ya kuwa mshirika wa kanisa, ubatizo ni jambo la muhimu sana kwa mmoja kuwa mshirika wa kanisa.

*6. Meza ya Bwana ni ishara ingine halisi ya mshirika wa kanisa*

Katika hoja ya pili tuliona kuwa agano jipya huja na ishara mbili. Ya kwanza ni ubatizo, ni kiapo-ishara ya kuanzisha agano. Ya pili ni meza ya Bwana, ambayo ni kiapo-ishara ambayo inafanya agano upya. Wakati tunakula pamoja mkate na kikombe, tunajitolea upya kwa Kristo na Agano lake jipya.

Na bado hi si kitu tunafanya pekee yetu kama mtu mmoja, lakini tunaifanya kama kanisa (1 Wakorintho 11:17-18; 20, 33-34). Na kushiriki meza ya Bwana inahushisha jukumu kwa kanisa. Kula na kunywa kwa njia ambayo isiyofaa, inafanya meza ya Bwana kutokuwa na maana inaofaa na huleta hukumu ya Mungu (1 Wakorintho 11:27,29). Kwa hivyo, kama tu vile tunajitoa kwa Kristo katika Meza ya Bwana, tunajitoa pia kwa kila mmoja. Kwa hilo tendo moja ambalo sisi tunashiriki na Yesu kama Mwokozi wetu, tunashiriki na kila mmoja kama ndugu na dada katika Kristo Yesu.

Hii inamaanisha kuwa Meza ya  Bwana ni ishara nyingine halisi ya ushirika wa kanisa. Kama vile Paulo anasema "Kwa kuwa mkate ni mmoja, sisi tulio wengi tu mwili mmoja, kwa kuwa wote twashiriki mkate mmoja" (1 Wakorintho 10:17). Meza ya Bwana haionyeshi tu umoja wetu, inathibitisha na kuweka muhuri huo wa umoja wetu. Meza ya Bwana hufanya wengi kuwa kitu kimoja kwa sababu inaazisha ushirika wetu na kila mmoja. Hii ndiyo sababu kuwa mshirika wa kanisa ni lazima ushiriki Meza, na mojawapo wa nidhamu ya kanisani  kutegwa kutoka kwa Meza.

Ubatizo ni muhimu kwa uwanachama wa kanisa kwa sababu hauwezi kushiriki kwa kiapo-ishara ya kufanya upya agano mpaka ushirikikwa kiapo-ishara ya kuanzisha agano. Huwezi shiriki kula chakula ya familia ya Meza ya Bwana kabla hujaingia kwa nyumba kwa kupitia mlango ya mbele ya ubatizo.

*7. Bila ubatizo huwezi kuesabiwa kuwa mshirika wa kanisa*

Je hii yote inaongeza nini? Ni hii tu: hatuwezi toa ubatizo kwa kile inahitajika kwa  ushirika wa kanisa kwa sababu bila ubatizo, mshirika haitakuwepo. “Ushirika” ni neno la theologia linaloonyesha uhusiano kati ya Mkristo na kanisa. Huu uhusiano wa kuwa mshirika wa kanisa unaokena wazi katika Agano Jipya wakati tunaona kwamba watu wengine huwa “ndani” na wengine huwa “nje” (1 Wakorintho 5:12).

Ubatizo na Meza ya Bwana huthibitisha uhusiano wa agano kati ya kanisa na mshirika wa kanisa. Kwa hivyo hakuna kitu kama mshirika bila ubatizo. Kuzungumzia mshirika bila ubatizo, ni kama kuzungumzia ndoa bila ahadi. Ndoa ni uhusiano ya agano inaofanywa na ahadi; mshirika ni uhusiano ya agano inaofanywa na kiapo-

ishara za ubatizo na Meza ya Bwana. Huwezi kuwa na uhusiano bila kiapo ambacho ni ubatizo. Kwa hivyo, huwezi kuwa mshirika bila ubatizo.

Ukweli kwamba ubatizo na meza ya Bwana ni ishara halisi ya mshirika wa kanisa, ni kumbusho kwamba tunapaswa kuzingatia kuwa mshirika wa kanisa kuwa jambo la muhimu sana. Mambo haya tufahamu kwamba hayawezi kutenganishwa kamwe. Ikiwa kuelewa kwetu juu ya kuwa mshirika wa kanisa hakuzingatii meza ya Bwana na ubatizo, mawazo yetu juu ya kuwa mshirika wa kanisa hayatakuwa ya Biblia. Katika Biblia kuwa mshirika wa kanisa inahusiano mkubwa sana na meza ya Bwana na ubatizo.

**Je, si jambo hili litawafanya wakristo wengi wakose kuwa washirika wa kanisa?**

Hii inamaanisha kwamba kila mtu ambaye anataka kuwa mshirika wa kanisa, anapaswa kubatizwa ikiwa ameokoka. Je, hii sitawafanya wakristo ambao walibatizwa wakiwa watoto kukosa kuwa washirika wa kanisa letu?

Wakristo wengi wanasema kwamba ikiwa mtu ameokoka, basi hiyo inatosha yeye kuwa mshirika wa kanisa. Wokovu ndio njia ya kuingia mbinguni na si ubatizo au meza ya Bwana. Swali ni je, kanisa litamjuaje Yule ambaye ameokoka? Ubatizo ni kukiri imani yako mbele ya wengi.

Kwa hivyo, ubatizo ni jambo la muhimu ambalo kanisa inatumia kujua kama mtu ni Mkristo, hata kama si hilo tu. Washirika wote wanaweza kuwa na uhakika kwamba mtu Fulani ameokoka, lakini ukweli ni kwamba Yesu anasema kwamba ndipo ajiunge na kanisa ni lazima abatizwe. Yesu hajapeana kanisa mamlaka ya kuthibitisha imani ya mtu mpaka hiyo imani itagazwe mbele ya watu kupitia ubatizo.

Kwa sababu ya umuhimu wa ubatizo, kanisa halijakubaliwa kumfanya mtu mshirika ikiwa hajabatizwa. Ikiwa kanisa linatafanya kinyume na mafundisho ya Yesu, litakosa kuweka mipaka halisi ya nani ameokoka nan i nani hajaokoka. Ubatizo unaweka mipaka katika kanisa na ulimwengu.

Ubatizo ni kitambulisho cha kuonyesha kwamba wewe umeokoka, kwa hivyo kukufanya ukubalike kuwa mshirika wa kanisa.

John Dagg mwalimu wa theologia alisema, “Kama vile kukiri kwa imani kunahitajika kwa mshirika wa kanisa, nidvyo ilivyo pia na ubatizo ambao ni sherehe maalum ya kukiri imani mbele ya wengine. Kukri kwa imani ndiyo hatua ya kwanza, halafu ubatizo ndiyo hatua ya pili. Wale wanaoamini ubatizo wa watoto wachanga wananyimwa ushirika kwa sababu siyo kuwa hawana hawajaokoka, lakini kwa sababu wamekataa kubatizwa. Kuwaza kwamba umebatizwa kwa sababu ya unawaza umebatizwa kweli, si kubatizwa. Hakuna kanisa ambalo linafaa kumfanya mtu kuwa mshirika ambaye hajabatizwa akiwa ameokoka. Si jambo zuri kukataa kumkubali mtu katika ushirika wa kanisa kwa sababu alibatizwa akiwa mtoto. Lakini ni jambo hatari zaidi kumleta katika ushirika wa kanisa akiwa anakataa kumtii Kristo. Hii itakuwa kupuuza mamlaka ya Kristo katika kanisa. Ikiwa mkristo analataa kutii Kristo Yesu, ni waza kwamba hatutaki kuendelesha kutotii kwake kwa kanisa lote.

## Kuweka mipaka

Yesu aliweka ubatizo, kwa sehemu, kutofautisha watu wake na ulimwengu.Ubatizo na Meza ya Bwana inayoonyesha, inakuza, na kuhifadhi injili kwa kutambua watu wa Kristo mbele ya watu.

Ubatizo inaonyesha kifo chetu kwa dhambi na ufufuo wetu kwa maisha mapya katika Kristo. Inatia muhuri kujitolea kwetu kwa Kristo na watu wake. Inaweka mipaka kati ya Kanisa na ulimwengu. Wakati huo huo ikialika wale ambao si wa jamii ya Mungu waje wawe wajiunge na jamii ya Mungu.  Ubatizo unaonyesha watu kwamba hivi ndivyo kanisa lilivyo.

Ubatizo huweka mipaka kati ya kanisa na ulimwengu, pia katika kanisa lote. Ubatizo hufunga mmoja kwa wengi. Inaongeza mkristo kwa kikundi cha hadharani ya watu wa Mungu duniani. Ubatizo basi ni ishara halisi ya mshirika wa kanisa. Ubatizo haionyeshi tu  njia ya kuingia kanisani; badala yake ubatizo ndiyo mlango wa mbele. Kwa kawaida, ubatizo huwapa mshirika wa kanisa.

Kwa sababu ya hizi sababu zote, ubatizo unahitajika kwa mshirika wa kanisa. Inaweza kuwa uko na nia ya kujiunga

na kanisa lakini hitaji ya kubatizwa kwanza umekufanya usitake kujiunga. Kama ni hivyo, ni imani yangu kuwa umeona sasa ya kwamba Yesu hakuhitaji kubatizwa tu, lakini pia anahitaji kanisa yake ikuhiaji ubatizwe. Na kama wewe ni kiongozi wa kanisa, ni imani yangu kuwa umeona ya kuwa kanisa inafaa kuhitaji wale wanadai kuwa Krsito ni Mwokozi wao kubatizwa- kama vile Yesu anahitaji.

## Je, ni wakati gani mtu anaweza kubatizwa, lakini awe kweli hajabatizwa?

Kusema kitu fulani kipo, ni lazima uwe unajua hicho kitu si kingine bali ni kile ambacho unakijua vizuri. Sura tatu zilizopita zimezingatia hasa juu ya ubatizo ni nini. Tutaendelea kuona kile ambacho si ubatizo. Tunafanya hivi kwa sababu, kuna wale ambao wamebatizwa na sasa wanaweza kuanza kuwa shaka juu ya ubatizo wao. Pili ni kwamba viongozi wa kanisa wanapaswa kuhakikisha kwamba washirika wao wanafahamu ubatizo nini. Kwa sababu hivi tutaona mambo manne ambayo yatatusaidia kuona, ubatizo ambao si wa kweli.

### Ikiwa ulibatizwa ukiwa mtoto mchanga

Tuliona katika sura ya tatu kuwa “ubatizo” ya watoto wachanga siyo ubatizo wa ukweli. Haijalishi vile hao wakristo ambao hubatiza watoto wachanga  wako na nia mzuri, na haijalishi zile sababu zao za biblia ya kufanya hivyo ziko, biblia haijatuamuru kubatiza watoto wachanga wa wakristo. Ubatizo ni ishara ya kuwa injili

imekuwa na athari kwa maisha ya mtu, huyo mtu ameunganika na Kristo. Ubatizo inaashiria ahadi iliyotimizwa.

Kwa hivyo kama ulibatizwa ukiwa mtoto mchanga, bado unahitaji kubatizwa kwa mara ya kwanza. Licha za juhudi mzuri ya kanisa iliyo "kubatiza", bado wewe uko ile hali kama mtu yeyote aliyekuja kwa Kristo na hajabatizwa.

**Ikiwa ulibatizwa ukidhani wewe ni mkristo, lakini haukuwa mkristo wakati huo**

Watu wengine walibatizwa kwa ruhusa yao wenyewe, wakichukulia tendo enyewe kama ukiiri wa imani kwa Kristo, lakini baadaye wanatambua kuwa hawakuwa wakristo wakati wa ubatizo. Angalia tukio hii:

Nilibatizwa nikiwa miaka 13 kabla sijaanza kutembea na Bwana. Ilikuja kama matokea ya kuangalia maada ya ubatizo katatika darasa la biblia ya vijana badaye tukaulizwa kama tungependa kubatizwa; Kuzingatia kuwa watu wengi waliokuwa kwa hiyo darasa walikuwa wanabatizwa, hata mimi niliamua nibatizwe. Nakumbuka wakati huo nilikuwa na aibu hata kuwambia marafiki

wangu wa shule kuhusu huo ubatizo, hata kuwauliza waje kushuhudia.

Mungu alifanya kazi kwa ukweli katika maisha yangu nikiwa miaka 20, na huo ndiyo wakati naweza sema Mungu alifungua macho yangu nikaweza kuona kufuata Yesu inamaanisha nini. Kwa hakika, hiyo ndiyo wakati ningebatizwa, lakini ni wazi kuwa nilikuwa nishabatizwa. Nigependa kusikiza maoni yako juu ya kubatizwa tena mara ya pili na kama unaona kubatizwa tena inahitajika.

Kwa hivyo huyu mtu - kwa urahisi wacha tudhani kuwa ni mwanaume- hakuwa anafikiria kuwa alikuwa Mkristo wakati alibatizwa. Ilifanyika “kabla sijaanza kutembea na Bwana.” Sababu yake ya kubatizwa ilikuwa ni kufanya kile ambacho umati ulikuwa inafanya: Wengi waliokuwa kwa hiyo darasa walikuwa wanaifanya.” Bali na kufanya ubatizo kama nafasi ya kujitolea hadharani kwa Kristo mbele ya yeyote anayetaka kujua, alijaribu kuinyamazia iwezekanavyo, bila kuambia rafiki yake yeyote wa shule. Na kutokana na maelezo yake, inakaa ni kama alikuja kuelewa ya ukweli kile kukuwa mwanafunzi wa yesu ilikuwa inamaanisha, na akamkristo Yesu kwa ukweli, miaka kadha badaye.

Kwa hivyo, huyu mtu anafaa kubatizwa tena, mara ya pili? Hapana, bila shaka hapana. Anafaa kubatizwa- kwa mara ya kwanza. Kama umebatizwa mara ya kwanza, umebatizwa. Lakini kama haukuwa Mkristo wakati “ulibatizwa” - kama, kulingana na maarifa yako, “ubatizo” wako haikuwa kukiri kwa kumwanini Yesu kwa ukweli na kujitolea kujiwasilisha kimkristofu kwa Kristo - basi “ubatizo wako” haikuwa ubatizo. Kama hii inaongea kukuhusu, unafaa kubatizwa.

Lakini kuna lingine lakujadili. Fikiria kuhusu stori ya huyu mwanamke mdogo (ni ya kufikiria, lakini ni ya kawaida sana).

Nililelewa katika nyumba ya kikristo. Wazazi wangu walinifundisha injili, na wakati nilikuwa na miaka sita, nilimba na baba yangu kuhusu kupokea Kristo. Nakumbuka kuhisi kushawishika kuhusu dhambi zangu na kujua kuwa alikufa msalabani ili kuniokoa. Nilibatizwa miezi kadhaa iliyofuata. Kutoka wakati, nilikuwa najua kuwa mimi ni Mkristo, na nilijua kuwa hiyo inamanisha kumkristo yesu na kuishi kulingana na neno lake.

Lakini katika miaka yangu ya ujana nilipitia kipindi ya shadi sana.Nilianza kuwa maswali kuhusu ukweliya

bibilia, na sikuwa napenda kile nilikuwa nasema. Wakati nilikuwa naomba, sikuwa nahisi kuwa Mungu alikuwepo. Si kuenda katika uasi mkuu, lakini mara nyingine maisha yangu ilikuwa inafanana na ya marafiki wangu ambaohawakuwa wakristo kuliko venye Mkristo alifaa kuishi. Mara nyingine nilidangaya kwa mtihani shuleni, na mara chache nilidanganya wazazi wangu kuhusu mahali nilikuwa naenda usiku ndiyo wasijue nilikuwa na marafiki wangu tukikunywa.

Leo sina uhakika ni wakti gani nilipata kuokoka. Katika miaka michache iliyopita nimehisi kuwa imani yangu imekuwa hai na nimekuwa kiroho kulingana na miaka kumi nyuma. Kwa sababu sijui kwa uhakika kama nilikuwa Mkristo wakati nilibatizwa, nafaa kubatizwa sasa, ili tu kuwa na uhakika?

Hii hali iko na kutoelewa  kwingi. Kwa mkono mmoja, huyu mwanamke mdogo alibatizwa kama jibu ya kusikiliza na inaonekana aliamini injili. Na inakaa kulikuwa na matunda ya Roho maishani mwake. Lakini tutafanya hizo miaka za ujana? Hakuacha kujiita Mkrist, lakini alikuwa anaishi kama Mkristo? Na sasa kwa sababu amekomaa, ako na wakati mugumu kufikiria kuwa binafsi

yake mdogo alimwani Kristo, kulingana na rekodi yake iliyochanganyika. Kwa hivyo anafaa kufanya nini?

Nitasema kuwa mtu ambaye alibatizwa kitambo kulingana na Ukiiri wake wa imani kwa Kristo anafaa "kubatizwa tena" kama anaamini sana kuwa hakuwa Mkristo wakati alibatizwa mara ya kwanza. Hatimaye, hiyo ni uamuzi mtu anafaa kufanya, kivyake, akisaidiwa na viogozi wa kanisa. Ubatizo inafaa kufanywa mara moja na haifai kurudiwa juu ya mashaka tu.

Katika jambo kama hili, inaonekana kama huyu mwanamke mdogo kwa hakika alielewa na kukubatia injili akiwa mdogo. Hata katika hizo miaka ya kuchanganyikiwa ya ujana, hakujiachilia kwa maisha ya kutotubu dhambi, na hakuwai kana imani yake kwa Kristo. Ni rahisi sana, kwa kuangalia kilicho fanyika hapo awali, kuchukulia kosa imani ya kitoto kuwa siyo imani kabisa na kuwekelea kiwango cha watu wazima ya matunda ya kiroho kwa mtoto au hata kijana. Hii ingekuwa majadiliano tofauti kama katika wakati moja kwa maisha yake alikana imani na kujiingiza katika hali mbaya ya dhambi ya hadharani bila kutubu. Kama ilivyo, nafikiri anafaa kuchukulia ukiiri wake wa imani ya hapo awali kama ya ukweli; lakini tena, hiyo ni uamuzi anafaa

kujifanyia. Nafikiri anafaa kutafuta ubatizo- na kanisa inafaa kumubatiza - kama tu ako na ushawishi kuwa hakuwa Mkristo wakati alibatizwa.

**Ikiwa kanisa ambalo lilikubatiza linakana injili**

Ubatizo ni alama ya injili. Kwa njia ya mchezo inaonyesha habari njema ya Kristo Yesu kupata na kuweka huru mwenye dhambi. Kubatizwa ni kutabulishwa na Yesu nakazi yake ya wokovu. Ubatizo basi inategemea injili kama hakuna injili, hakuna ubatizo.

Kama kila Mkristo angeamuriwa kubatiza kwa sababu tu ya kuwa Mkristo, kanisa haligekuwa katika hii hali. Lakini, kwa sababu Yesu ameamuru kanisa kufanya tangazo maalumu duniani kwa niaba mbiguni, kwa hivyo katika hali ya kawaida, ni kanisa pekee ambalo lina mamlaka ya kubatiza. Na ni mwili tu ya wakristo ambao inathibitisha na kutangaza injili inafaa kujiita kanisa.

Mara nyingine mukusanyiko ya wanao kiiri imani hujiita “makanisa’ lakini wameondoka kwa ukweli wa injili mpaka wanaikana. Kwa mfano, kama kanisa inafunza kuwa kifo cha Yesu ilikuwa tu dihirisho ya upendo Mungu alihitaji kwa wanadamu, na ufufuo wake haikuwa

ya kimwili lakini hisia ya kiroho kwa mioyo ya wanafunzi wake, hiyo kanisa itakuwa imebadilisha injili na injili ya uongo. Na kama vile Paulo anasema, injili nyingine ambayo kwa kweli si injili kamwe (Wagalatia 1:6-7).

Makanisa mengine kwa ufanisi hukana injili kupitia imani zao kuhusu ubatizo. Kwa mfano, kama kanisa itachukulia ubatizo kuwa kama kitu cha kuokoa na abacho inapeana msamaha wa dhambi na kuzaliwa upya, basi hiyo kanisa imeweka ubatizo  mahali pa injili. Ubatizo na injili hazifayi kuwa kutenganishwa: Yeyote anayeamini ameamuriwa kubatizwa, na ubatizo inashuhudia na kutangaza injili. Lakini ubatizo haifayi kutambuliswa na, au kuchukuliwa kwa niaba ya injili.

Kanisa ambalo kwa ufanisi inakana injili siyo kanisa kabisa, ambayo inamanisha kuwa hawana amri kutoka kwa Kristo ya kubatiza watu kwa jina lake. Kwa hivyo “ubatiz” ambayo inafanywa na kanisa ambayo inakana ubatizo kwa ukweli si ubatizo.

Kama hii hali ni ukweli, tutawezaje kujua kama kanisa iliyokubatiza kwa kweli inakana injili? Ni ngumu. Kama uko na tuhuma kuwa hii inaweza kuwa hali yako,

nitakuhimiza kuuliza viongozi wa kanisa lako ya sasa kukusaidia kuweza kujua.

Kwa uwazi: hakuna kanisa ambayo iko na mafudhisho kamilifu, na hakuna mhubiri ambao haiwezi kosea. Sisemi kuwa ubatizo ni halali tu kama kanisa iko mafundisho iliyo asilimia 100 kamilifu.  Na sisemi kuwa kama muhubiri mwenyewe hatakuwa mkristofu kwa injili ambayo anahiburi, ya kuwa ubatizo ambazo amezifanya zinakuwa halali. Badala yake, nasema kuwa ile injili ambao huazisha kanisa, ndiyo injili ambayo hupewa kanisa mamlaka na nguvu ya kubatiza na kubatizwa. Sina haja na yule mtu anayefanya ubatizo lakini nina haja  na kanisa inayoiamuru hiyo ubatizo. Ili kanisa ibatize, inafaa kuthibitisha na kutagaza injili ya biblia.

**Je, ubatizo unahusiana kwa njia yoyote na kanisa?**

Hali ya mwisho ambayo tutangalia ndiyo ngumu kuliko zote kutabua. Ubatizo unaofanyika bila uhusiano wowote na kanisa kabisa. Acha tufanye njia yetu kupitia hali mbili zisizo za kawaida. Kwa upande moja, uko na ubatizo ambao ulifanywa na Mchungaji katika kusanyiko la kanisa linaohubiri injili. Hakuna shida hapo. Kwa upande mwingine, wacha tufanye hali yetu ya kuzamishwa kwa

maji kutoka sura wa kwanza kuwa ya kisasa. Uko kwa kisima cha kuongelea ya rafiki yako katika mkusanyiko ya majira ya joto. Nyinyi wote ni wakristo -kwa kweli, rafiki yako ndiye alikuogoza kwa Kristo wiki chache zilizopita.

Anasema, “Habari, haujabatizwa bado, au?
“Hapana. Nadhani nifaa kubatizwa.”
“Kwa nini usifanye hivyo saa hii? Naweza kukubatiza.”
“Um, sawa”
Kama wakati huo rafiki yako atakuingiza kwa maji na aseme haya maneno, “ Nakubatiza kwa jina ya Baba, Mwana na Roho Mtakatifu,” utakuwa umebatizwa? Tofauti na ile hali ya kuzamishwa ya ukurasa wa kwanza, hapa umekubali kufanya hivyo. Kwa ukweli ulikuwa umekuja kwa imani kwa yesu hivi karibuni. Na rafiki yako anajua ya kwamba umemkristo Kristo kwa sababu ni yeye alikuhubiria injili.Lakini hizi sababu hufanya hio tendo kuwa ubatizo?

Nigepedekeza kuwa katika hali mingi, jibu ni la. Kumbuka kuwa katika ubatizo, mtu hujitolea kwa Kristo na watu wake, na kanisa huthibitisha ukiiri wa imani ya mkristo. Lakini hakuna maana ya rafiki yako kutenda kwa niaba ya kanisa. Hakuna maana ya kanisa kusemezana

kwa jina la Yesu wakati rafiki yako anakuzamisha kwa maji. Hii ndiyo shida ya uamuzi hapa, kitu ambacho kinakosekana ndipo hii hali iweze kutimiza kuwa ubatizo.

Hata hivyo, nilisema “kwa hali nyingi”. Kama uko mahali ambapo hakuna kanisa kwa sababu hakuna Wakristo, ningesema kuwa mtu yeyote aliye na injili yuko na mamulaka ya kubatiza. Kama hakuna kanisa la mtaa, basi kila Mkristo, kama ilivyo, anabeba mbegu ya kanisa pamoja naye- hiyo mbegu ikiwa injili, ambao inapadwa kwa kuitagaza. Tutaongea mengi kuihusu katika sura unaofuata. Kwa sasa maoni yangu ni kuwa kama ni mahali ambapo hakuna kanisa, mtu yeyote anayehubiri injili anaweza na anafaa kubatiza wale wanaoamini injili.

Lakini katika hadith ya kuzamishwa kwa maji kwenye kisima cha kuongelea, hiyo siyo hali iliyopo. Kuna makanisa mengi karibu.Rafiki yako ni mshirika wa moja. Kwa hivyo, badala ya kuchukuwa jukumu ya kukufanya mwanafunzi kwa mkono zake, anafaa kukuweka kwa kanisa ikushugulikie. Ulipo kuja kwa Kristo, anafaa kusema, “ Vizuri, sasa wacha nikutabulishe kwa watu wa Kristo.Kuna makanisa mengine aminifu katika jiji letu, lakini hii ndiyo yangu. Acha tuongea na mchungaji wa

kanisa kuhusu vile itakuwa kwa wewe kubatizwa na kuungana na kanisa.

Tena, mahali ambapo kanisa la mtaa iko, ubatizo siyo na uhusiano na kanisa siyo ubatizo. Kumbuka ubatizo ni taarifa na vikundi viwili, siyo moja- Mwenye anabatiza na yule anabatizwa. Na kwa sababu kanisa iko mahali hapa, lakini kanisa haijaongea kwa njia yeyote kwa niaba ya Yesu, hi kuzamishwa haijatimiza kuwa ubatizo. Ni kanisa tu iko na mamlaka ya kuapisha raia kwa ufalme.  Ni kanisa tu liko na mamlaka ya kupeana kiapo-ishara ya kuanzisha agano jipya. Ni kanisa tu lina mamlaka ya kusema, “Tazama hapa kila mmoja:Huyu ni wa Yesu.”

Inamaanisha nini kwa ubatizo kukuwa na uhusiano na kanisa ya mtaa? Tutatazama mengi ya haya katika sura inayofuata, Lakini kwa kuchungulia, nafikiri kuna uwekano ya mabadiliko hapa. Sifikirii kuwa Maandiko yanaamuru mchungaji kubatiza, ingawa nafikiria ni busara kufanya hivyo. Sifikiri kuwa Maandiko yanaamuru ubatizo ufanyike katika mkusanyiko wote wa kanisa. Ingawa tena, nafikiri kuwa ni busara na inaambatana vizuri na kazi ya ubatizo kwa kuonyesha kujitolea kwa mwili na thibithisho la mwili. Kwa hivyo, kama siyo lazima kwa mchungaji kufanya ubatizo katika

mkusanyiko wa kanisa, basi hiyo inaacha nafasi kidogo ya mabadiliko kwa jinsi ubatizo inafaa kufanywa kihalali.

Bado, kuna ubatizo ambao unahusiana na kanisa nan i wa kweli. Pia kuna ule ambao hausiani na kanisa na huo si wa kweli. Hali zingine ziko wazi njia moja au nyingine. Lakini siyo zote. Kwa mfano, rafiki wangu wa karibu kwa kweli alibatizwa na rafiki yake, katika kisima cha kuongelea. Walikuwa katika kambi ya kikristo, na watu wengi walikuwa wanabatizwa. Hii ni ubatizo halali? Sina uhakika. Kama nakumbuka vizuri, kambi ilikuwa na uongozi fulani wa kanisa, lakini sijui jinsi kanisa ilikuwa limehusika au halikuhusika katika ubatizo. Ubatizo ni lazima uweke mipaka.  Kwa sababu ilifanyika hadharani, siyo kwa siri, na kwa sababu kulikuwa na uhusiano fulani wa kanisa ingawa kwa umbali, niko tayari kukubaliana nao kiasi.  Lakini inaweza ona kwa urahisi jinsi kanisa itafanya maamuzi ambao ni  kinyume.

Hatimaye, hii ndiyo mifano ya maamuzi makanisa ya mitaa inafaa kufanya wakati wanathamini wanao taka ubatizo. Kwa upande mmoja, hatutaki kuweka viwango vikali kushinda vya Maandiko. Kwa upande mwingine hatutaki kuacha ubatizo uwe kitu cha siri na kutolewa kwa kanisa, na kuinyima kanuni ya kufanya wanafunzi,

kuweka mipaka, kazi ya kufanya ya kanisa. Hii inahitaji hekima na ufahamu wa biblia.

Hii pia inahitaji utambuzi  kwa upande wa Wakristo. Kama umekuja kwa Kristo hivi karibuni, au kuongoza mtu kwa Kristo hivi karibuni, hakikisha ya kwamba mahali ya kwanza ya kuanza kufanya uamuzi ni kanisa. Kanisa ni mwili ambayo Yesu amechangua kutenda na kuongea kwa niaba yake, inayowakilisha ufalme wa mbiguni duniani. Na kanisani ni mahali ambapo wanafunzi wanakuwa kwa pamoja katika ukamilifu wa Kristo (Waefeso 4:11-16). Mkristo mpya ataenda wapi siku yake ya kwanza kazini? Kanisa la mtaa.

**Yanayofuata na ya Mwisho**

Hii sura imeangalia juu ya kile ambacho si ubatizo ili kuonyesha wazi ukweli. Kama yale ambayo umepitia yanaabatana na hali ambazo tumejadhili kwa sura hii, ni matumaini yangu kuwa umetoka na dhamira safi ikiwa umetimiza amri ya Yesu ya kubatizwa. Ikiwa haujabatizwa unafaa kubatizwa. Na kama wewe ni kiongozi wa kanisa, ni matumaini yangu kuwa umeelewa wazi ubatizo ni nini na ubatizo siyo.

Lakini, kwa uhakika, makanisa hayatambui tu ubatizo, pia wanabatiza watu. Kwa hivyo katika sura yetu inayofuata, na ya mwisho, tutangalia swali, “ Ni njia ipi kanisa inafaa kufanya ubatizo?”

## Je, ni wakati gani mtu anaweza kubatizwa, lakini awe kweli hajabatizwa

Kwa Wakristo wengi, kitu ya maana wanastahili kufanya na ubatizo,ni kubatizwa. Kwa uhakika tunafaa kuangazia kwa ubatizo wetu ili kutukubusha kuwa tumeunganiswa na Kristo, na kuwa sasa tumepewa nguvu na amri ya kuishi maisha mapya (Warumi 6:1-4). Na kama tuko na nafasi, tunafaa kuwahimiza na kuwarai Wakristo wengine kubatizwa kama hawajafanya hivyo. Lakini kulingana na utii wako kwa Yesu, kama ushabatizwa, ni hayo tu.

Kwa viongozi  wa Kanisa, hadithi ni tofautu kabisa. Kanisa nyiingi ambayo hubiri injili kwa kawaida  huwa na nafasi ya kubatiza wakristo wapya, kwa kawada ni viogozi wa kanisi ndiyo hubatiza. Lakini kufanya ubatizo ambao huleta maswali mingi: Ni maji kiasi gani inafaa kutumiwa? Kumwangia au kuyunyuzia mtu maji ni mzuri kama kumzamisha? Ni nani anafaa kufanya  ubatizo? Ubatizo  una uhusiano gani na mshirika wa kanisa? Makanisa wanastahili kubatiza watu wapi na wakati gani?

Mtu anafaa kuchukua muda gani baada ya kuja kwa Kristo ndipo abatizwe?

Hii sura inashugulikia maswali haya yote, kwa mpangilio ambao nimetaja. Nikiziweka kwa ufupi, tunaenda kuangalia jinsi ya kufanya ubatizo, nani anafaa kubatiza, matokeo ya ubatizo,hali ambayo ubatizo inafaa kufanyiwa, na wakati wa kufanya ubatizo. Ni imani yangu kuwa wale ambao siyo viongozi wa kanisa watahisi umuhimu wa hizi maswali. Kama haujabatizwa, hii sura itakusaidia kukagua jinsi na mahali pa kutafuta ubatizo. Kama umebatizwa hii sura iakusaidia kusaidia wengine wapate kubatizwa kwa njia inaolingana na Maandiko.

Mwishowe, neno kwa wale ambao siku moja watakuwa waenezaji wa injili, wakihubiri injili mahali ambapo kanisa halipo. Kwa sababu mawaidhi yangu katika hii sura yanahusu mahali ambapo tayari kanisa lipo, hayahusu ubatizo wa kwanza mahali ambapo kanisa linaanza. Lakini ikiwa unatii amri kuu ya Yesu ya kuwafanya watu kuwa wanafunzi wa Yesu, na unawafunza kutii amri zote, basi utafundisha wale ambao wameokoka kwamba kumfuata Yesu ni kuanzisha makanisa. Yesu anasema, “Kwa kuwa wanapokusanyika pamoja watu wawili au watatu kwa Jina langu, mimi niko

papo hapo pamoja nao” (Mathayo 18:20). Hii inamaanisha kuwa wakati tu utakuwa na zaidi ya moja ya wakristo wapya, na unafaa kuwaongoza hawa wakristo kuazisha kanisa. Mara tu hao wakristo wapya watakuja kwa Kristo,wanastahili kuishi kama kanisa, kwa kuangalia ubatizo wa wakristo wapya. Kwa hivyo hii sura ni muhimu kwa wamisiyonari kama ilivyo kwa viongozi wa kanisa ambazo zimekomaa.

## Njia ya Ubatizo

Makanisa wanahitaji maji kiasi gani ili kubatiza mtu? Wanastahili kujenga ama kuomba mahali kubwa ya kuzamisha watu, au chombo cha maji iliyojengwa kanisani au jagi kubwa inatosha?
Katika sura 1 tuliona kuwa neno la kigiriki ya baptize inamaanisha kurushwa kwa maji au kuzamishwa chini ya maji. Yohana alikuwa anabatiza watu katika  Ainoni kuli kuwa na maji mengi huko (Yohana 3:23), na towashi wa kushi aliuliza kubatizwa wakati aliona bwawa la maji kado ya barabara (Matendo ya Mitume 8:36). Ni kwa ajili ya hiyo ubatizo, towashi wa kushi na Filipo “wakateremuka” Kwenye maji na halafu “walipanda”kutoka kwenye maji (Matendo ya Mitume 8:38-39). Inawezekana kuwa waliteremuka kwenye maji

halafu Filipo akachukuwa maji kutumia mikona yake na kumwangilia mwenzake, lakini haya haiwezekani. Haielezi kwa nini towashi aliomba abatizwe wakati alipoona bwawa kubwa la maji. Na kwa nini hawa wanaume wote walipitia shida ya labda kutoa nguo zao au kujilowa kama kuzamishwa haikuwa inahitajika?

Zaidi, kuzamiswa inaonyesha vizuri ishara ya kuzikwa na kufufuliwa na Kristo. Katika Warumi 6:1-4 na Wakolosai 2:11-12, Paulo anachukulia kama kitu cha kawaida kuwa ubatizo inaonyesha muungano na kifo, kuzikwa, na kufufuliwa kwa Kristo. Hitimisho ya busara ambayo wasomaji wake watafikiria wakati waliwekwa chini ya maji halafu wakatolewa nje, siyo wakati walinyunyuziwa au kumwagiliwa maji.

Kwa hivyo ningesema ya kwamba inatuonyesha kuzamishwa kama njia ya kawaida ya kubatiza watu. Hii siyo tu kitu Wakristo wa kitambo walifanya na kuwa tuko na fursa ya kuachana nao kama tunapenda. Badala yake , njia ya ubatizo imefugwa na ishara na manufaa ya ibada; kwa hivyo makanisa wanastahili kuchukua hatua zozote ambao ni muhimu ili kubatiza watu kwa kuzamisha.

## Msimamizi

Inayofuata, ni nani anahitajika kufanya ubatizo? Kama ubatizo ni tendo la kanisa, basi msimamizi wake lazima amepatiwa mamlaka na kanisa. Yule anayefanya ubatizo anatenda kwa niaba ya kanisa, wala si kwa mpango yake wala kwa mamlaka yake.

Kanisa kwa jumla wanatimiza funguo za ufalme lakini mtu mmoja ndiyo amepewa jukumu la kubatiza. Ubatizo bado ni zoezi ya funguo la ufalme. Ubatizo ni kitu rasmi ambao kanisa linatambua kwamba mtu anadai kumfuata Kristo. Katika ubatizo kanisa linaongelesha kuhusu Kristo na mbatizaji anahitajika kuongea kwa niaba ya kanisa.

Wachungaji ambao pia wanaitwa viongozi au waangalizi katika maandiko walichaguliwa kufundisha na kuongoza kanisa (1 Tim 3:1, 5:17). Wachungaji wametambuliwa katika kanisa kwa ajili ya zoezi la uangalizi kanisani. Wanafundisha neno, kuhimiza kanisa kutii neno, kuwa mfano mzuri katika uaminifu wa neno na kuongoza maisha ya kanisa kulingana na neno la Mungu. Ningependa kupendekeza ya kwamba wakati maandiko haihitaji ubatizo kufanyiwa na mchungaji, ni lazima iwe hivyo. Wachungaji au waangalizi ni wale wanaotenda

ubatizo kwa niaba ya kanisa kama wanavyofundisha neno, na ubatizo ni ibada ya washirika wote na hivyo kutambua ya kwamba neno ilihubiriwa na likapokelewa. Na siamini ya kwamba hii inamaanisha ya kwamba mchungaji pekee anayesitahili kubatiza badala yake ninafikiria kila mchungaji au mwaangalizi yuko na mamlaka ya kubatiza waamini.

Vile nilivyosema sifikiri ya kwamba kuwa mchungaji pekee ndiye anayehitajika kubatiza.  Hata hivyo kama kanisa inanuia kuwamrisha wengine kubatiza, nafikiria ni lazima waangalie kwa umakini ni nani na kwa nini na vipi. Kwa mfano, kama kanisa inaruhusu mara kwa mara akina baba kubatiza watoto wao, ya kwamba kwa kiasi kikubwa kanisa inatuma ujumbe ya kupotosha ya kwamba ubatizo ni kanuni ya familia na siyo ya kanisa.

Lakini kitu muhimu sana ni kwamba ubatizo ni tendo la kanisa siyo ya mkristo binafsi ambayo inamaanisha ya kwamba msimamizi wake amepewa uwezo na kanisa. Mkristo wa kawaida hana mamlaka ya kuwabatiza wakristo kanisani.

Kama vile nilivyosema kwa sura iliyopita, ya kwamba penye hazipo makanisa, hali ni tofauti. Kama wewe ni

mkristo pekee katika jiji, wewe ndiye kanisa katika huo mji. Haimaanishi ya kwamba unatenda kulingana na mpango wako kibinafsi kando ya mamlaka ya kanisa. Badala yake unabeba na kupanda mbegu ya kanisa ambaye ni injili. Mahali ambapo mbegu ya injili inazaa matunda ya imani na toba na unapaswa kuratibu huo upokelezi na ubatizo. Wakati unapokuwa na watu wawili au watatu wamekusanyika katika jina la Yesu na ni lazima uwafundishe kanisa changa ya kwamba ubatizo ni tendo ambao wako na jukumu ya kufanya na kusimamia. Na ni lazima ufanye ubatizo zijazo kwa usimamizi na kwa niaba yao.

## Matokeo

Ubatizo ni tendo la kanisa la kuthibithisha na kuonyesha muungano wa mkristo na Kristo kwa kumuzamisha ndani ya maji, na ni tendo la mkristo ya kujitoa hadharani kwa Kristo na watu wake, kwa hivyo kuunganisha mkristo na Kanisa na kumtofautisha na dunia. Katika ubatizo mkristo hujitolea kwa watu wa Mungu, na watu wa Mungu hujitolea kwa Mkristo. Kwa hivyo mahali ambapo kuna kanisa, ubatizo unafaa kufanywa na washirika wa kanisa. Kanisa ambayo inafanya ubatizo inafaa, na hilo tendo, inafaa kumuigiza huyo mkristo mpya katika orodha yao.

Ubatizo siyo tu kitu inayohitajika kabla ya mshirika wa kanisa; kwa kawaida, ubatizo uazisha mshirika wa kanisa. Mshirika wa kanisa ndiyo nyumba, na ubatizo ndiyo mlango wa mbele.

Hali tu ambayo hiyo inaweza kutofanyika  yenye naweza ona ni kama mkristo mpya anaodoka kwenda mahali ambapo haina kanisa. Kwa mfano, Mkristo mpya ambaye anaweza kuwa anaelekea kuishi kwa meli kwa mwaka moja. Ama mtu ambaye anafanya kazi kwa biashara ya kimataifa anaweza kuwa anaenda Mashariki Ya Kati na hana habari ya kuwepo kwa kanisa huko. Hali hizi si za kawaida, lakini saa zingine hatuwezi kuzikwepa. Hawa waamini wanajipata katika hali inayofanana na ile ya towashi wa Kushi. Kwa hivyo kwa hizi hali ambazo kwa ukweli si za kawaida, kanisa inafaa kuwabatiza, kuwaombea, kuwatuma na kuwahimiza kutafuta ushirika wowote ya wakristo wanaweza pata wakati watakakuwa wakitembelea mataifa. Na tumeangalia hali ya wale wanaoenda na kueneza injili mahali hakuna makanisa. Ule mkristo wa kwanza wa hiyo mahali habatizwi ndani ya kanisa, lakini mara tu moja au wawili watabatizwa wanastahili kuanzisha kanisa.

Katika kesi zile zingine, ubatizo na mshirika wa kanisa hazifai kugawa. Hakuna mtu anafaa kubatizwa kama hauko tayari kujitolea kukuwa nchini ya mamlaka ya Yesu na kujitolea kwa kanisa lake. Hii thibitisho ambalo linapeanwa kama pasipoti linafaa kuambatana na jukumu na uajibikaji wa uraia. Kwa mkristo mpya, ubatizo inafaa kuwa njia ambayo na wakati ambayo mtu hujiunga na kanisa. Kama mko na hatua ambazo inajumuisha mafudhisho, mahojiano na kura ya wanakanisa, mtu anafaa kupitia hizi hatua kabla hajabatiza. Na kanisa inafaa kuelewa kuwa mshirika inapeanwa katika ubatizo.

Zaidi ya hao, makanisa hawafai kuigiza wakati wa kungojea kati ya ubatizo na mshirika. Wengine wanaweza fanya hivyi kwa minajuili ya kusisitiza ubatizo. Wanangawanyisha ubatizo na mshirika wa kanisa kwa nia ya kulete uangalifu kwa ubatizo. Lakini njia ya biblia ya kusistiza ubatizo ni kuifanya mlango ya kuingia ndani ya kanisa  na kwa hivyo kuingia katika maisha ya Ukristo. Kwa upande mwingine, wengine wanaweza ingiza nafasi kati ya ubatizo na mshirika kwa sababu mshirika inaleta majukumu mengi, na inaweza kuwa mkristo mpya hayuko tayari kutekeleza hayo  jukumu. Shida ya hiyo ni kuwa, kila Mkristo anahitajiwa na kuwezesha na Mungu kuchukua nafasi yao kwa mwili. Kwa hivyo kama uko

tayari kuthibitisha kuwa mtu ni Mkristo, hakuna sababu ya kumuweka nje ya mwili. Hapo tu ndiyo mahali anaweza nawiri, jukumu na zote. Na kama uko na tashwishi kuhusu kama mtu yuko tayari, labda unapaswa kujiuliza kweli kama uko tayari kukubali imani ya mtu huyu kupitia ubatizo.

Katika hali za kawaida, ubatizo na mshirika wa kanisa yanafaa kuwa pamoja. Kitheologia ubatizo humpa na mtu kuwa mshirika wa kanisa. Kwa hivyo haufai kubatiza watu bila kuwaleta katika ushirika wa kanisa, na unafaa kupeana mshirika kwa wale wote unaowabatiza.Mshirika wa mkristo mpya inafaa kukuwa hali inayohitajika wakati mtu anapo batizwa na inafaa kuanza kazi wakati wa ubatizo.

## Ubatizo unastahili kufanyika wapi

Makanisa yanapaswa kuwabatizia watu wapi? Je inastahili kufanyika katika jengo la kanisa au katika ibada ya kanisa? Siyo lazima. Maandiko ni kama inakubalia ubatizo ifanyike ndani au nje ya ibada ya kawaida kanisani na tunaona mifano baadaye ya agano jipya. Lakini tunaweza kusema zaidi ya haya?

Ubatizo ni kukiri imani kwa umma, na kanisa ni la kwanza na ni mahali muhimu ambapo kukiri imani unapohutubiwa. Kwa kuwa ubatizo ni kazi ya kanisa kwa jumla katika kuhakikisha muumini amekiri na amekaribishwa katika hesabu ya ukristo. Naweza kupingana kwa kawaida ya kwamba makanisa wabatize wafuasi wao katika uwepo wa kusanyiko la washiriki wao wote. Ikiwa kundi hilo limekusanyika kanisani au kwa mto haijalishi. Kitu muhimu ni kwamba zoezi ya ubatizo kanisani isiwe ya kujificha lakini ya kuonyesha kwamba kanisa linaongea kwa niaba ya Mungu kwa watu binafsi na watu banafsi wanaongea kwa niaba ya Mungu na kanisa kwa jumla.

Kubatiza kwa kusanyiko lote la kanisa inatangaza kwamba; kubatiza kusanyiko la kundi ndogo inanyamazisha ubatizo.

Kufikiria “wamisheni wa frontier” nilikuwa nataka kupendekeza umati, kupita kwa mbatizaji si lazima kwa ibada ya washirika kanisani, tangu mbatizaji mwenyewe amekuwa shahidi kwa washirka kupitia kukiri kwake kwa imani. Na hiyo ‘kusanyiko ya mmoja’’ ubatizo unakubalika tu wakati shahidi wengine haupatikani.

Ubatizo lazima usherekewe na kanisa lote kwa sababu ni tendo la kanisa.

## Wakati

Mwishowe, Makanisa wanastahili kubatiza watu baada ya muda gani? Lazima wakristo wapya wabatizwe mara moja au kunafaa kuwa na wakati wa kungojea?

Kwa uhakika, mifano yote ya ubatizo tuko nao katika agano jipya ilifanyika mara tu mtu alikuja kwa imani. (angalia kwa mfano, Matendo ya Mitume 2:38:41; 10:47-48; 16:14-15, 30-34; 19-15). Na kwa sababu ubatizo ni mahali imani hudhihiriswa hadharani, inafaa kuhusishwa na kubadilika kwa mtu kwa karibu iwezekanovyo. Kwa hivyo, kwa upande moja makanisa yanafaa kuweka muda wakungojea kabla kubatiza mtu ili kupima matunda ya imani ya mtu ama kumufudhisha misingi ya maisha ya imani ya kikristo na mazoea kabla kumbatiza.
Lakini kama ubatizo inafaa kupeana mshirika wa kanisa, hatufai kushughulika kuhusu jambo ya kuwa kanisa inachelewesha ubatizo kwa wiki kadha au hata miezi kadha? Hii siyo kuchelewesha ubatizo au kuwa kinyume na mtindo katika biblia? Sivyo hasa. Hatua za kuwa mshirika wa kanisa haikuwi wakati wa kuchelewesha.

Badala yake, inahakikisha kuwa yule mtu anayetaka kubatizwa anajua kile anaenda kufanya na kanisa inamujua mtu anayeenda kubatizwa.

Wakati wa Pentecoste, ilikuwa wazi kabisa kile ulikuwa unaamua kufanya: Upinganizi kutoka kwa viongozi wa wayahudi na maisha mpya kati ya wafuasi wa Yesu waliokuwa wakiteswa. Siku hizi, vitu haziko wazi vizuri. Kuna watu ambao wanakiri ukristo ambao wanafikiria kuwa kuwa Mkristo haina uhusiano na kujitolea kwa utawala wa Yesu na haina uhusiano na kanisa lla mtaa. Kanisa inafaa kuhakikisha kuwa wale ambao wabatizwa wanajua kuwa kuishi maisha ya Ukristo uko na uhusiano yote na kujitolea kwa utawala wa Yesu na uhusiano wote na kanisa. Yale ambayo yanafanyika wakati mtu analetwa katika ushirika wa kanisa, yanadhihirisha wazi umuhimu wa ubatizo. Haya yanahakikisha kuwa wale wanaofanya ahadi katika ubatizo, yaani kanisa na mkristo, wanajua kile wanaahidi na wanaahidia nani. Kufanyia wale wanaotaka kubatizwa kupitia hatua hizi ndipo wawe washirika wa kanisa inasaidia kuhakikisha kuwa ubatizo unaweka mipaka ya ukweli kati ya kanisa na ulimwengu. Hii inaonyesha kujitolea kwa mkristo kwa Kristo na watu wake, na  inatimiza lengo la Yesu la kutofautisha watu wake kwa kuwatabulisha na Yeye.

Kwa hivyo, kwa kuwa wazi, sifikiri kuwa makanisa ya dini ukristo zilizo Magharibi, hasa kwa yale ymebaki katika msingi wa bibilia, wanastahili kufanya mikutano ambayo mtu yeyote anaweza kuja mbele na abatizwe mara hiyo hiyo, bila kujitolea kuwa mshirika wa kanisa. Kukiri kwao hakufai kwa siri bali kwa hadharani ili waajibike kwa Kristo na watu wake.

Kama unaishi katika nchi ya Waisilamu ambapo kubatizwa inamaanisha kukataliwa na familia yako, hali iko wazi vizuri. Lakini hasa kwa wale ambao wako America, njia ya busara ni kuhakikisha kabla ya wakati mkristo anajua kile ambacho anaenda kufanya. Na makanisa wanahitaji kuhakikisha kuwa kile wale wanaobatizwa wanakubali kufanya ni ushirika wa kanisa na maisha ya kuishi chini ya mamlaka ya Kristo.

## Umuhimu

Katika kitabu hiki dogo tulianza na maoni ya biblia kuhusu ubatizo na tumemalizia kwa zile vitu zinashikilia ubatizo. Kupitia haya yote tumeona kitu ya nani, nini, wakati gani, wapi na hasa sababu ya ubatizo. Kama wewe ni mkristo katika Yesu na maswali yako kuhusu ubatizo

zimekufanya kususia ubatizo, ni tumaini langu kuwa hiki kitabu kimejibu haya maswali na imefungua njia kwa wewe kumtii Yesu kwa kujitolea hadharani kwake na kwa watu wake katika ubatizo. Kama wewe ni kiongozi wa kanisa, natumaini umepata usaidizi wa kuelewa ubatizo, kufundisha kanisa habari za ubatizo, na kuongoza kanisa yako katika zoezi la ubatizo.

Ni nini inafanya ubatizo kuwa kitu cha maana? Ubatizo inawekea watu wa Mungu muhuri na ishara ya injili. Inaonyesha kujitolea ya mkristo hadharani kwa Kristo, ikimuweka katika njia ya kimaisha ya kuwa shahidi wazi wa neema ya Mungu katika injili. Inawekea muhuri kujitolea kwa mkristo kwa Kristo na watu wake, na kumuweka katika ushirika wa mwili wa Kristo. Inaongea neno la thibitisho na kukubaliwa kutoka kwa kanisa kwa mkristo kwa niaba ya Kristo. Haya yote ndiyo sababu Yesu aliamuru wanafunzi wake kubatiza na kubatizwa.

Ubatizo inaonyesha na kukuza injili. Na ubatizo hutofautisha na kuweka mipaka kati ya watu wa injili, yaani wale ambao wametubu dhambi na kumwamini Kristo. Ubatizo ni muhimu kwa sababu ya injili ambayo ubatizo inaashiria.